# Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Wizara ya Maji, Nishati na Madini

## Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2026/2027


ILIYOWASILISHWA NA

**MHE. NADIR ABDUL-LATIF [AL-WARDY]**

WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI







**MEI, 2026**

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027

**ILIYOWASILISHWA NA**


**MHE. NADIR ABDUL-LATIF AL-WARDY**
**WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI**


**MEI, 2026**

## YALIYOMO

YALIYOMO ........................................................................................ i
ORODHA YA VIAMBATISHO ................................................................ ii
VIFUPISHO VYA MANENO ................................................................. iii
A. UTANGULIZI ........................................................................... 1
B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI –MACHI, 2025/2023 ........................................ 3
C. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI-MACHI 2025/2026 ........................................................... 25
D. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027................................ 41
E. HITIMISHO.................................................................................. 47

# ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Namba 1: Muhtasari wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........ 50
Kiambatisho Namba 2:Mapato yatokanayo na Maliasili Zisizorejesheka kwa mwaka 2025/2026 ........ 52
Kiambatisho Namba 3: Vijiji vilivyopatiwa huduma ya umeme ........ 53
Kiambatisho Namba 4: Maeneo yaliyokuwa na tatizo la umeme mdogo ambayo yameshapelekewa ya huduma za umeme ........ 54
Kiambatisho Namba 5: Hali ya uingizwaji na matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa (Julai - Machi) 2025/2026 ........ 55
Kiambatisho Namba 6: Vituo vya mafuta kwa kipindi cha Julai - Machi, 2026 ........ 56
Kiambatisho Namba 7: Mwenendo wa bei za Mafuta zilizotangazwa na Mamlaka kwa kipindi cha Julai- Machi, 2025/2026 ........ 57
Kiambatisho Namba 8: Gesi iliyoingizwa na kutumika kwa kipindi cha Julai -Machi, 2026 ........ 58
Kiambatisho Namba 9: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini ........ 59
Kiambatisho Namba 10: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ........ 71

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CCTV | Closed Circuit Television |
| EPC+F | Engineering, Procurement, Construction + Finance |
| GRB | Gender Responsive Budget |
| IPF | Investment Project Financing |
| kV | Kilovoti |
| MW | Megawatt |
| NEC | National Energy Center |
| TZS | Tanzania Shillings |
| USAID | United State Agency for International Development |
| VAT | Value Added Tax |
| WASH | Water Sanitation and Hygien |
| ZPDB | Zanzibar Presidential Delivery Bureau |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muweza wa yote, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Lengo letu kuu ni kuendelea kuimarisha huduma na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu atujalie busara na hekima katika kujadili hotuba hii ya bajeti pamoja na bajeti kuu ya Serikali kwa ujumla.

2. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake thabiti na juhudi zake katika kuleta maendeleo Nchini. Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha dhamira ya dhati ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora ya maji safi na salama pamoja na nishati ya uhakika kupitia utekelezaji wa miradi mbali mbali nchini. Hali hii inaakisi kauli mbiu yake isemayo "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Kazi Iendelee."

3. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake mahiri katika kusukuma mbele maendeleo ya Zanzibar, hususan katika sekta za maji na nishati. Tumeshuhudia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo maji, afya, elimu, barabara za kisasa na masoko, jambo linalodhihirisha kasi ya maendeleo na utekelezaji madhubuti wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2025-2030).

4. **Mheshimiwa Spika,** ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Maji, Nishati na Madini. Naahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujituma ili kuhakikisha wananchi wote wa Zanzibar wananufaika na huduma za maji safi na salama, nishati nafuu na endelevu pamoja na usimamizi bora wa rasilimali za madini.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, kwa uongozi wake na mchango wake katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Hotuba yake imeweka dira na mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali na kuthibitisha kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar isemayo "Yajayo ni Neema Tupu." Ni dhahiri kuwa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2020–2025) umefikia mafanikio makubwa na sasa tunaendelea kwa kasi zaidi kutekeleza Ilani ya 2025–2030.

6. **Mheshimiwa Spika,** ninakushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma, Naibu Spika, kwa uongozi wenu mahiri. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa juhudi zao za kuwatumikia wananchi na ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

7. **Mheshimiwa Spika,** ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA, Mheshimiwa Mihayo Juma N'Hunga pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mwanaidi Kassim Mussa na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuendelea kutoa ushauri na kuhakikisha ushirikiano wa karibu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Maoni na ushauri wao yamezingatiwa kikamilifu katika bajeti hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** aidha, kwa dhati kabisa ninampongeza Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Seif Kombo Pandu, kwa ushirikiano wake. Vile vile, nawapongeza Katibu Mkuu, Ndugu Joseph John Kilangi, Naibu Katibu Mkuu, Bi. Mwanajuma Majid Abdullah, pamoja na viongozi na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake, wakiwemo ZURA, ZECO na Rand Water Zanzibar, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi. Kwa pamoja tunaahidi kuendelea kuwatumikia wananchi kwa weledi na juhudi ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji, umeme na Maliasili Zisizorejesheka ipasavyo.

9. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. Ushirikiano huu umechangia mafanikio makubwa katika sekta mbali mbali za maendeleo nchini.

10. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa imani yao juu ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, hususan katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 kwa kukipatia ushindi wa kishindo Chama Cha Mapinduzi. Naendelea kuwahimiza kudumisha amani, umoja na mshikamano ili kuendeleza kasi ya maendeleo katika Awamu hii ya Nane.

11. **Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara yamezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-2050, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22– 2025/26), Ilani ya CCM (2025–2030) pamoja na Sera, Sheria, Kanuni na maoni ya wadau mbali mbali.

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, naomba uniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2025/2026

***Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026.***

***Upatikanaji wa Fedha***

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Maji, Nishati na Madini (Fungu N03) iliidhinishiwa kutumia **TZS. 220.82 bilioni**, kati ya fedha hizo **TZS. 2.44 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), **TZS. 2.92 bilioni** kwa ajili ya Mishahara (PE), **TZS. 10.11 bilioni** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara ya ZAWA na **TZS. 205.35 bilioni** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

    Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 Fungu N03 liliingiziwa jumla ya **TZS. 87.15 bilioni** sawa na asilimia **39.47**. Kati ya fedha hizo, **TZS.798.01 milioni** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia **32.73, TZS. 2.11 bilioni** kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **72.55, TZS. 6.72 bilioni** ruzuku ya mishahara ya ZAWA sawa na asilimia **66.48** na **TZS. 77.52 bilioni** sawa na asilimia **37.75** zimetumika kwa kazi za miradi ya maendeleo. ***Kiambatisho Namba 1 kinahusika.***

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara kupitia Maliasili Zisizorejesheka, ilipangiwa kukusanya **TZS. 20.75 bilioni**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 15.29** bilioni sawa na asilimia **75** ya makadirio ya mwaka na wastani wa asilimia **98.26** ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa. Mafanikio haya yanatokana na usimamizi na udhibiti mzuri wa maliasili zisizorejesheka. ***Kiambatisho Namba 2 kinahusika.***

***Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai – Machi, 2025/2026***

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilitekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vikuu vitano (5) vilivyo chini ya Programu Kuu tatu (3) kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kuboresha upatikanaji wa huduma za maji, nishati na madini;
ii Kuongeza rasilimali na uwezo wa Taasisi katika kudhibiti na kusimamia huduma za maji na nishati;
iii. Kuboresha usambazaji na upatikanaji wa huduma za maji safi na salama, nishati pamoja na rasilimali za madini;
iv. Kuendeleza tafiti kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta zilizo chini ya Wizara; na
v. Kutekeleza na kusimamia miradi mikubwa ya kimkakati.

***Sekta ya Maji Nchini***

16. **Mheshimiwa Spika,** maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya viumbe wote wanaoishi duniani, Maendeleo yote duniani ikiwa ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa yanategemea upatikanaji wa huduma ya maji. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa mstari wa mbele kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma ya maji safi na salama katika shughuli za kila siku.

17. **Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, sekta ya maji inaendelea kukabiliwa na changamoto mbali mbali zinazotokana na ongezeko la mahitaji ya maji. Ongezeko hili linachangiwa na sababu tofauti zikiwemo kuongezeka

kwa idadi ya watu, kukua kwa miji pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kama vile uwekezaji na utalii. Aidha, mabadiliko ya tabianchi, uvamizi wa vyanzo vya maji, uchakavu wa miundombinu, pamoja na mwitikio mdogo wa baadhi ya wananchi katika kuchangia huduma ya maji.

18. **Mheshimiwa Spika,** tunaamini kuwa changamoto hizi zinaweza kutatuliwa iwapo kutakuwa na ushirikiano wa dhati kati ya Serikali na wananchi. Aidha, ni muhimu kwa kila mmoja kubadili mtazamo na kutambua kuwa mchango wa kila mwananchi katika kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji na miundombinu yake ni msingi katika kufanikisha azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wote.

19. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na juhudi zinazoendelea, ikiwemo utekelezaji wa miradi mbali mbali ya sekta ya maji, kiwango cha uzalishaji wa maji kimeongezeka kutoka wastani wa lita milioni 211 na kufikia wastani wa lita milioni 218 kwa siku, sawa na asilimia **86.5** ya mahitaji kwa mwaka 2025/2026. Hata hivyo, mahitaji halisi ni lita milioni 252 kwa siku, hali inayopelekea kuwepo kwa upungufu wa takriban lita milioni 34 kwa siku katika maeneo ya Unguja na Pemba.

20. **Mheshimiwa Spika,** ongezeko la kiwango cha uzalishaji wa maji limetokana na juhudi mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, ikiwemo kukamilika kwa miradi mipya ya maji, uchimbaji wa visima vipya, pamoja na ufungaji wa pampu katika visima vya zamani ili kuongeza ufanisi wa uzalishaji. Vile vile, ujenzi na ukarabati wa matangi ya kuhifadhia maji pamoja na upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji vimechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa huduma ya maji kwa wananchi.

21. **Mheshimiwa Spika,** aidha, hali ya miundombinu ya maji na mtandao wa usambazaji inaendelea kuimarika na kukidhi viwango vya ubora wa maji vya kitaifa, ingawa bado kuna changamoto ya uchakavu wa mabomba katika baadhi ya maeneo.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara inaendelea kuchukua hatua madhubuti ikiwemo kupeleka mtandao mpya wa mabomba katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya maji pamoja na kubadilisha mabomba chakavu ili kuongeza ufanisi na kupunguza upotevu wa maji.

***Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji***

23. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo imekasimu majukumu yake kwa Kampuni ya *Rand Water Zanzibar*. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 programu hii iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 165.51 bilioni** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ruzuku ya mishahara ya wafanyakazi wa ZAWA, mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, **TZS 154.55 bilioni** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, **TZS 10.11 bilioni** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, **TZS 307.43 milioni** kwa ajili ya mishahara na **TZS 543.01 milioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 programu hii imetumia **TZS. 14.47 bilioni**. kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS 7.40 bilioni** sawa na asilimia **5** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, **TZS 6.72 bilioni** sawa na asilimia **66.48** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na **TZS 211.10 milioni** sawa na asilimia **69** kwa ajili ya mishahara na **TZS 144.44 milioni** sawa na asilimia **45** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

***a) Idara ya Maendeleo ya Maji***

24. **Mheshimiwa Spika,** sekta ya maji ni muhimu kwa maendeleo na ndio mhimili wa afya kwa umma na ustawi wa jamii, Serikali imeendelea kuwekeza ili kuhakikisha wananchi na wakaazi wananufaika na huduma ya maji safi na salama.

25. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kukamilisha Mradi wa Ukarabati wa Miundombinu ya Maji Kengeja-Pemba uliogharimu **TZS 1.29 bilioni**, ikiwemo ukarabati wa tangi la maji la lita 300,000, uchimbaji wa kisima

kipya na ulazaji wa mtandao wa mabomba kilomita 13.7. Aidha, mradi umeunganisha nyumba 1,850 kwa kuwapatia huduma ya maji safi na salama, hivyo imepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya maji katika Shehia ya Kengeja, Chole na vijiji jirani. Mradi huu ulikamilika Disemba, 2025 na kuzinduliwa rasmi tarehe 02 Januari, 2026 katika maadhimisho ya miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuandaa andiko la mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji wa Mkoa wa Kusini Unguja, ikiwa ni jitihada ya kuhakikisha changamoto ya upungufu wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama inaondoka. Mradi huu utaimarisha usambazaji wa maji safi na salama katika Mkoa wa Kusini Unguja kupitia uwekezaji katika mfumo wa EPC+F.

27. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji SJMT kupitia Mamlaka ya Maji DAWASA, inaendelea na ujenzi wa tangi la ujazo wa lita 1,000,000 katika Kijiji cha Kizimkazi, ambapo tangi hili linatarajia kutatua changamoto ya maji katika Shehia za Kizimkazi Dimbani na Mkunguni. Kazi hii ina tarajiwa kukamilika ndani ya mwezi Juni, 2026 na imegharimu jumla ya **TZS. 2.9 bilioni.**

28. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kulinda vyanzo vya maji kwa kuondoa majaa yasiyo rasmi karibu na vyanzo vya maji kwa maeneo mbali mbali Unguja na Pemba ambayo yangeleta madhara ya kuchafua maji. Jumla ya majaa 11 yameondoshwa Unguja (Magharibi "A" saba (7) Mwanyanya Chemchem, Kihinani, Kianga, Kijichi, Mwera, Hawai na Mtoni, Magharibi "B" manne (4); Maungani, Kisauni, Fuoni Migombani na Sokoni). Kwa upande wa Pemba maeneo manne (4) ambayo ni Taifu, Gawani, Chanjaani- Konde na Kijichame - Sizini.

29. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kutekeleza Sera ya Maji na Usafi wa Mazingira ya 2025 imeanzisha Jumuiya za uhifadhi wa rasilimali maji ngazi ya Shehia za majaribio katika maeneo matatu ya vianzio vya maji ambayo ni Bububu- Chemchem, Kisauni na Maungani, kwa lengo la kudhibiti wimbi la uvamizi, uharibifu wa miundombinu ya maji, udhibiti wa uanzishwaji wa shughuli zinazopelekea uchafuzi wa mazingira katika

maeneo ya vyanzo vya maji pamoja na ulinzi shirikishi kwa ngazi ya jamii. Jumuiya hizo zina wajumbe 12 ambao ni;(Sheha wa Shehia, Askari jamii-mmoja (1), Wajumbe wa Sheha wawili (2), Wanajamii watano (5), Afisa-mmoja (1) kutoka Manispaa/Halmashauri husika, Afisa- mmoja (1) kutoka Wilaya husika na Afisa mmoja (1) kutoka Idara ya Maendeleo ya Maji). Sambamba na hilo, Wizara inaendelea na uandaaji wa muongozo wa uendeshaji wa Jumuiya za kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji pamoja na jinsi ya ufanyaji wake kazi kwa ngazi ya Shehia.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kudhibiti ubora wa maji pamoja na kuhakikisha matumizi sahihi na endelevu ya rasilimali hiyo kwa jamii, Wizara imefanikiwa kukamilisha zoezi la kuviwekea vibati vya utambuzi visima binafsi 2,643 vilivyopo katika Wilaya ya Magharibi A. Aidha, zoezi hilo linalenga kuvisajili visima hivyo ili kuwezesha ufuatiliaji wa karibu na usimamizi madhubuti wa matumizi ya maji.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kupunguza uvamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji, Wizara imefanikiwa kukamilisha zoezi la uwekaji wa mabango 18 pamoja na viguzo vya fensi kwa vyanzo tisa (9) Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja vyanzo vitano (5) (Donge Mbiji, Mkorogo, Msikiti Mzuri, Mjonga na Kwarara), na kwa upande wa Pemba vyanzo vinne (4) (Pujini, Kengeja, Vitongoji Changuo na Chamanangwe).

32. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara imefanikiwa kukarabati ukuta katika eneo la Chanzo cha Maji Mwanyanya Chemchem, hatua ambayo imesaidia kulinda rasilimali hii muhimu. Kazi hizi zimelenga katika kuhakikisha usalama wa vyanzo vya maji na kuimarisha mazingira ya huduma za maji safi na salama.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na utaratibu wa utoaji wa vibali vya malipo ya uchimbaji wa visima vya watu binafsi pamoja na leseni ya usajili kwa wachimbaji na kampuni za uchimbaji visima ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa Sera ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka, 2025. Aidha, Wizara imekamilisha Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa za Maji Safi na Maji Taka (Kanzidata), *Zanzibar Water and Wastewater Information System* (ZanWWIS). Mfumo huo tayari umezinduliwa na kuanza kutumika na unawezesha kupata taarifa mbali mbali zinazohusu maji safi na maji taka.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kukusanya na kuchambua taarifa za mfumo wa maji taka katika Wilaya ya Mjini, ambapo jumla ya maeneo 27 yametambuliwa yakitumia mfumo wa mtandao wa maji taka "Sewer System" unaomwagaa maji taka baharini pamoja na maeneo mengine yanayotumia makaro majumbani. Utambuzi huu umeiwezesha Wizara kufahamu hali halisi ya mfumo uliopo kwa ajili ya kupanga usimamizi na maboresho yake.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Rasilimali Maji Chini ya Ardhi, yenye wajumbe 12 kutoka Wizarani na sekta za nje ikiwemo; Elimu, Mazingira, Hali ya Hewa, Utafiti, Ardhi, Tawala za Mikoa na Kilimo. Kamati itakuwa na jukumu la kufanya tafiti, kutoa mapendekezo, kutoa miongozo ya kulinda rasilimali maji, kutoa elimu kwa umma na kushirikiana na wadau mbali mbali katika usimamizi bora na endelevu wa rasilimali maji chini ya ardhi.

36. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya maji ni pamoja na uvamizi katika maeneo ya vyanzo vya maji hususan maeneo ya Maungani na Kisauni-Kwarara, kukosekana kwa baadhi ya vifaa vya kiutendaji ikiwemo vifaa vya kutosha vya upimaji maji, kutokuwepo kwa mfumo wa usimamizi wa rasilimali maji chini ya ardhi pamoja na kukosekana kwa miongozo ya kiutendaji katika usimamizi wa maji taka.

37. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua za utatuzi ikiwa pamoja na kuandaa programu maalum ya kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kuvijengea uzio na kuiwasilisha programu hiyo Tume ya Mipango Zanzibar kwa ajili ya kupatiwa fedha, kutayarisha Mpango wa Mahitaji ya vifaa vya upimaji na usimamizi wa rasilimali maji kupitia mradi wa Water-IPF unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

***Sekta ya Nishati Nchini***

38. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar inaendelea kupata huduma ya umeme kupitia waya tatu za chini ya bahari kutoka Tanzania Bara. Kwa upande wa Unguja inatumia waya wa 45MW ulowekwa mwaka 1980 na waya wa 100MW ulowekwa mwaka 2013 zote kutoka Ras- Kiromoni hadi Ras-Fumba. Kwa

upande wa Pemba, inatumia waya wa baharini wenye uwezo wa 20MW kutoka Majani Mapana Tanga hadi Ras Mkumbuu, ambao unaendelea kutumika hadi sasa.

39. **Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa huduma ya umeme Zanzibar unaendelea kuimarika, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026, jumla ya uniti 745,162,000.00 kWh zimepokelewa kutoka Tanzania Bara, jumla ya uniti 573,850,644.00 kWh zimeuzwa kati ya 719,624,670.00 kWh zilizopangwa, sawa na asilimia 80 ya mauzo. Hii imepelekea mauzo ya jumla ya **TZS. 154.59 bilioni** bila kujumuisha tozo ya VAT.

40. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi haya yanatokana na kiwango cha umeme kinachopokelewa Unguja kwa kuzingatia uwezo wa miundombinu ya waya iliyopo. Hata hivyo, mahitaji halisi ya umeme kwa sasa ni takribani MW 165, hivyo kuna upungufu wa karibu MW 30. Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya umeme, upungufu huo unakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa MW 40 kila mwaka. Endapo jitihada zinazoendelea za kupata umeme wa ziada hazitafikia malengo yaliyokusudiwa, upungufu huo unatarajiwa kufikia takribani MW 70 katika mwaka wa fedha 2026/2027.

41. **Mheshimiwa Spika,** aidha, kumekuwa na tatizo la kukatika kwa umeme kutokana na changamoto zifuatazo: -

i. ***Kuzidiwa kwa mtandao wa kusambazia umeme:*** Zanzibar inaendelea kushuhudia ukuaji wa kasi wa maendeleo unaotokana na ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kimkakati katika sekta mbali mbali ikiwemo; barabara, utalii, afya na elimu. Hata hivyo, ukuaji huo hauendi sambamba na maboresho ya miundombinu mipya ya umeme.

ii. ***Athari za kimazingira:*** laini nyingi za kusafirishia na kusambazia umeme zimezungukwa na mazingira hatarishi ikiwemo; kupitiwa na miti mikubwa, hali inayopelekea baadhi ya wakati kukosekana kwa huduma ya umeme kwa laini hizo kunatokana na kuangukiwa na miti hiyo hasa kipindi cha mvua kubwa na upepo mkali.

iii. ***Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara:*** Ujenzi wa barabara umekuwa ukiathiri miundombinu ya usambazaji wa umeme iliyopo juu na chini ya ardhi.

42. **Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto hizo hususan ya umeme hafifu Zanzibar, Wizara kupitia ZECO imechukuwa hatua zifuatazo: -

i. Mradi wa kuzalisha 30MW za umeme wa jua kupita kampuni ya "Generation Capital ltd" katika eneo la Bambi ambapo kwa sasa tayari baadhi ya vifaa vimeshawasilishwa eneo la mradi, ambapo majaribio ya mwanzo yanatarajiwa kufanyika mwezi Julai, 2026.

ii. Mradi wa kuzalisha 30MW za umeme wa jua na Betri za kuhifadhia umeme zenye uwezo kuhifadhi 20MWh, kupitia kampuni ya "Eleckmeck" ambapo kwa sasa tayari ushaanza utekelezaji na unatarajiwa kukamilika Disemba 2026.

iii. Mradi wa kuzalisha umeme wa upepo 200MW ambao unatekelezwa na kampuni ya "Assel Tanzania Ltd" ambapo kwa sasa wapo katika hatua ya ukusanyaji wa takwimu za upepo (wind parameters).

iv. Mradi wa kusafirisha umeme wa 270MW kupitia waya wa Baharini kutoka Tanzania Bara hadi Zanzibar, na waya wa 100MW kutoka Majani Mapana Tanga hadi Pemba, mradi unaosimamiwa na Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) kwa kushirikiana na ZECO unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Kwa sasa mradi upo katika hatua ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakao athirika na mradi huo pamoja na kukamilisha taratibu za kumpata Mshauri Elekezi (PMC) ambaye atasimamia utayarishaji wa nyaraka kwa ajili ya utafutaji wa mkandarasi wa ujenzi. Matarajio ya kukamilika kwa mradi ni Disemba, 2028.

v. Mradi wa Kuimarisha Sekta ya Nishati na Ufikiwajiwa Huduma ya Umeme (ZESTA), ambao unajumuisha uzalishaji wa umeme wa jua wa 18MW pamoja na betri za kuhifadhia umeme zenye uwezo wa kuhidhi 40MWh. Mradi wote kwa ujumla unatarajiwa kukamilika Agosti, 2027.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Wizara imeingia tena mkataba na Kampuni ya Novavis International Ltd kuendelea kuimarisha mfumo wa umeme Zanzibar. Mradi utajumisha kuunganisha njia no. 1 (45MW) ya mkondo wa 132kV kuiunganisha na mfumo wa STATCOM (Static Synchronous Compensator) katika eneo la Mtoni, ambapo kwa njia no. 2 (100MW).

Mradi huu umekamilika na kuleta matokeo chanya kwa kutuhakikisha voltage ya umeme kutoka Tanzania Bara inakuwa thabiti na ya kutosha. Aidha, Kampuni hii pia itaimarisha miundombinu ya umeme na kuweka mfumo wa ufuatiliaji (DMS) ili kuondosha tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kwa upande wa Pemba.

**44. Mheshimiwa Spika,** vile vile, Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha miundombinu ya kusambaza umeme kwa kuongeza njia mpya za usambazaji umeme kwa lengo la kupunguza mzigo kwenye laini zilizopo na kuongeza ufanisi wa usambazaji wa umeme. Njia hizo ni kama ifuatavyo: -

i. **Njia ya kusambaza umeme kutoka mtoni hadi Selem,** ambayo inalenga kupunguza mzigo kwenye laini ya Kaskazini kongwe na mpya, hivyo kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Mtoni,Mbuzini, Seaclif, Kitope, Mwakaje hadi Selem na Bumbwini;

ii. **Njia ya kusambaza umeme kutoka Shakani hadi Chukwani,** ambayo inalenga kupunguza mzigo kwenye laini ya Mazizini;

iii. **Njia ya kusambaza umeme kutoka Mpendae hadi Jang'ombe,** ambayo inalenga kupunguza mzigo kwenye laini ya Jang'ombe; na

iv. **Njia ya kusambaza umeme kutoka Pongwe ya Uroa hadi Kiwengwa,** ambayo inalenga kupunguza mzigo kwenye laini ya Kaskazini hadi Kusini na kuweka njia mbadala kwa watumiaji.

**45. Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa njia hizi mpya za usambazaji kutasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara na hivyo kuongeza ufanisi na uendelevu wa huduma kwa wananchi.

**46. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto ya ongezeko la mahitaji ya umeme, Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kupanua mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha 33kV na 11kV. Katika kipindi cha Julai-Machi, 2025/2026, jumla ya urefu wa mtandao wa kusafirisha umeme uliojengwa ni kilomita 48.96 hii ni sawa na asilimia 142 ya mpango uliowekwa wa kujengwa kilomita 34.5 katika kipindi hicho. Aidha, kwa upande wa mtandao wa umeme mdogo, Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kujenga kilomita 225.75 kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025/2026. Hii ni sawa na asilimia 272 ya mpango uliowekwa wa kujengwa kilomita 83 katika kipindi hicho.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za muda mrefu, Wizara kupitia Mradi wa ZESTA inatekeleza ujenzi wa laini ya Usafirishaji umeme wa 132 kV ambayo itasafirisha umeme katika maeneo ya Kaskazini na Kusini Unguja. Ujenzi huo unaenda sambamba na ujenzi wa Vituo vya kupoozea umeme katika eneo la Makunduchi- Mkoa wa Kusini na eneo la Matemwe- Mkoa wa Kaskazini. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa laini hizo na Vituo vya kupoozea umeme tayari wapo eneo la kazi na kazi inaendelea.

***Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini***

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kupitia Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ambayo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 52.00 bilioni** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo **TZS 50.79** bilioni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, **TZS 889.11 milioni** kwa ajili ya mishahara na **TZS 316.94 milioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 programu hii imetumia **TZS70.39 bilioni** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, **TZS 70.11 bilioni** sawa na asilimia 138.03 kwa ajili ya miradi maendeleo, **TZS231.29 milioni** sawa na asilimia 26 kwa ajili ya mishahara na **TZS 49.50 milioni** sawa na asilimia **16** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

***b) Idara ya Nishati na Madini***

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sekta ya Nishati na Sekta ya Madini ikiwemo matumizi endelevu ya maliasili zisizorejesheka kupitia mifumo hiyo ya kisera na kisheria, Wizara inatakiwa kuhakikisha upatikanaji wa Maliasili Zisizorejesheka kwa mwananchi mwenye uhitaji unafanyika kwa ufanisi ili kupunguza athari za mazingira zinazoweza kujitokeza.

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini, katika kutekeleza jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka, 2025, imeandaa Mpango Kazi wa Sekta ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 unaolenga kutekeleza malengo makuu sita (6), ambayo ni: -

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka, 2025;
ii. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya nishati, ikijumuisha nishati Jadidifu, nishati sanifu na nishati za kisasa ikiwemo nishati safi ya kupikia;
iii. Kushiriki katika mikutano, warsha na makongamano ya kikanda na kimataifa yanayohusu masuala ya nishati;
iv. Kufanya tafiti kuhusu vyanzo mbalimbali vya nishati;
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kupitia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu; na
vi. Kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya nishati.

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa elimu ya matumizi bora ya nishati safi ya kupikia katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Shehia, kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia na nishati jadidifu. Elimu hiyo ilitolewa kupitia skuli na makundi maalumu ya vijana.

52. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara ilikutana na wadau wa sekta ya nishati kutoka Taasisi za Serikali, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kwa lengo la kutoa elimu na kukusanya maoni kuhusu matumizi bora ya nishati na nishati safi ya kupikia. Kupitia kikao hicho, wadau walitoa maoni yao ikiwemo: -

i. Kutengeneza sheria maalumu kwa watumiaji wakubwa wa nishati chafu za kupikia na kubadilisha nishati hizo kuwa nishati safi za kupikia;
ii. Kuingiza mada mahususi za elimu katika skuli juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na matumizi sanifu kwenye mitaala ya ngazi ya msingi na sekondari;
iii. Kupunguza tozo na kodi za uingizaji wa mitungi na vifaa vinavyohusiana na nishati safi ya kupikia na sanifu ili kuhamasisha matumizi ya vifaa hivyo; na
iv. Kuwepo na mfumo wa utoaji wa ruzuku kwa watumiaji wakubwa wa nishati ya kupikia ili kuwasaidia gharama za awali.

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki na kuratibu vikao, makongamano na warsha mbali mbali za sekta ya nishati ndani na nje ya Zanzibar, hatua iliyowawezesha watendaji kubadilishana uzoefu, kupata maarifa mapya ya teknolojia na sera pamoja na kuimarisha ushirikiano na wadau wa sekta. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililoandaliwa na *Mwananchi Communication Ltd* Septemba, 2025 jijini Dar es Salaam, ambapo Wizara iliwasilisha jitihada za Serikali katika kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuchapisha makala maalum kuhusu mikakati ya kukabiliana na matumizi ya nishati chafu katika gazeti la Mwananchi.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu vikao vya ugeni wa *Taasisi ya Global Green Energy* kutoka Korea Kusini tarehe 5 hadi10 Septemba, 2025 kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa mradi wa umeme wa jua unaotarajiwa kutekelezwa katika Hospitali ya Binguni na vijiji jirani; vile vile, ilishiriki semina ya kitaalamu ya "Ubadilishaji wa Takataka kuwa Nishati" iliyoandaliwa na Taasisi ya Wahandisi Tanzania tarehe 4 na 5 Septemba, 2025 Zanzibar.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine Wizara imeshiriki katika warsha ya Maadhimisho ya Siku ya Usafi Duniani iliyoandaliwa na WEZA, ikihusisha shughuli za usafi na ugawaji wa majiko ya gesi kwa wananchi ambapo Wizara ilipata nafasi ya kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia; pamoja na kushiriki katika mkutano wa Bodi ya Wahandisi Tanzania (ERB) uliofanyika Dar es Salaam tarehe 24 hadi26 Septemba, 2025, uliosaidia kuongeza uelewa kwa wataalamu wa Wizara kupitia masuala ya kiufundi na teknolojia mpya.

56. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka, 2025 na kuendeleza juhudi za upatikanaji wa umeme na nishati mbadala. Katika juhudi za kuondoa matumizi ya kuni na mkaa na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inaendelea kuandaa Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Zanzibar. Mkakati huo utatoa muongozo wa matumizi ya nishati safi na salama kwa ajili ya kupikia na kuendeleza juhudi za kupunguza mabadiliko ya tabianchi, magonjwa ya upumuaji na kuimarisha ustawi wa jamii wa Wananchi.

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imeshiriki vikao vya kufuatilia miradi na kutafuta misaada kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Ofisi za Umoja wa Ulaya Tanzania (EU) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (UNCDF). Kupitia vikao hivyo, EU iliridhia kufadhili Upembuzi Yakinifu wa ubadilishaji wa waya mkongwe wa baharini wa 45MW na kutoa mkopo ambao utakua na msaada wa asilimia 20 ya mkopo kwa ajili ya ulazaji waya mpya wa 100MW.

58. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ikishirikiana na Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TANESCO na ZECO imeendelea kushiriki katika vikao vya maandalizi ya mpango wa Tanzania kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya nyuklia. Kupitia vikao hivyo, mpango wa utekelezaji wa miaka sita na nusu umeandaliwa, jumla ya vinu vinne(4) vya kuzalisha umeme wa nyuklia vitajengwa, ambapo kinu kimoja kati ya hivyo kimependekezwa kujengwa Zanzibar na kinatarajiwa kuzalisha megawati 300 za umeme.

59. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliimarisha uwezo wa watendaji wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi. Mafunzo hayo ni pamoja na mafunzo ya uelewa wa bima za nishati yaliyolenga kulinda uwekezaji na kupunguza hatari za kifedha katika miradi ya nishati, pamoja na mafunzo ya uandaaji wa Mikataba ya Mauziano ya Umeme (PPA) yaliyowezesha kuandaliwa rasimu za mikataba ya uzalishaji umeme kwa kutumia nishati ya jua, upepo, mafuta na gesi asilia.

60. **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 01 Oktoba, 2025, Wizara ilizindua Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar uliotekelezwa na Kampuni ya *Novavis International ya Marekani*. Mradi huu ulihusisha ufungaji wa vifaa vya kudhibiti na kuimarisha voltage, ikiwemo voltage regulators katika maeneo nane (8), kati ya hayo matano (5) Unguja na matatu (3) Pemba; capacitor banks katika maeneo 31, yakiwemo 26 Unguja na matano (5) Pemba; pamoja na mfumo wa STATCOM katika eneo la Mtoni. Utekelezaji wa mradi huu umeimarisha kwa kiasi kikubwa uthabiti na ubora wa umeme katika gridi ya umeme ya Zanzibar.

*Sekta ya Madini*

**61. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepewa jukumu la kusimamia Sekta ya Madini ikiwemo matumizi endelevu ya Maliasili Zisizorejesheka kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Namba 3 ya Mwaka, 2015 pamoja na Kanuni ya Matumizi Endelevu ya Maliasili Zisizorejesheka ya Mwaka, 2011, ili kutoa huduma kwa wananchi wenye uhitaji na miradi ya kimkakati kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

**62. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa ikitoa vibali na leseni za uchimbaji na usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka pamoja na gari zinazotumika kusafirisha Maliasili hizo. Aidha, Wizara huhuisha maeneo yaliyochimbwa Maliasili Zisizorejesheka, kudhibiti uchimbaji na usafirishaji haramu kupitia doria pamoja na kufanya tafiti za jiolojia na madini ya Zanzibar.

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuendelea kusimamia uchimbaji na usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka imekagua maeneo matatu (3) yaliyoombewa vibali vya kuchimbwa kifusi ambapo eneo moja kati ya hayo limepatiwa leseni ya uchimbaji. Aidha kupitia ukaguzi huo, Wizara imetoa vibali vya kusafirisha mawe na udongo katika maeneo 24 pamoja na ufunguzi wa machimbo nane (8) ya mchanga kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi na miradi ya kimkakati.

**64. Mheshimiwa Spika,** Wizara inakiri uwepo wa uchimbaji haramu wa Maliasili Zisizorejesheka. Hata hivyo, Wizara inapenda kuwakumbusha kwamba jukumu la ulinzi wa Maliasili hizo, ni suala la mtambuka kuanzia kwa wananchi, Uongozi wa Shehia, Wilaya na Mkoa pamoja na Taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kudhibiti uchimbaji haramu, Wizara imeweka vituo vya ukaguzi katika maeneo yote ya Unguja na Pemba, ambapo vituo (25) vya Unguja na (10) Pemba. pamoja na kuendelea kufanya doria katika maeneo yote. Aidha, Wizara imekuwa ikiwachukulia hatua kwa wale wote wanaokiuka sheria na miongozo iliowekwa.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka, 2011 kifungu Na. 6 gari zote zinazosafirisha Maliasili Zisizorejesheka zinatakiwa kupimwa ili kujua kiwango cha upakizi (haulage capacity) kabla ya kupatiwa leseni. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeendelea kupokea maombi ya kupima gari zinazosafirisha Maliasili Zisizorejesheka ambapo hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2025 jumla ya gari 654 Zimeshapimwa na kupatiwa leseni kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi, miradi ya kimkakati na viwanda vya matofali na kokoto.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na hatua za ulipaji wa fidia kwa wananchi waliochimbiwa mchanga kupitia mfumo wa zamani baada ya kujiridhisha na madai husika kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambayo kwa wakati huo ndio iliyokua ikisimamia shughuli za uchimbaji ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 kiasi cha Jumla ya **TZS. 509.30 milioni** zimelipwa kwa wananchi watano (5) waliowasilisha madai yao na kuhakikiwa katika maeneo ya Donge mtu mmoja (1) na Pangatupu watu wanne (4).

67. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na Jiolojia ya Zanzibar tunakabiliana na upungufu mkubwa wa mchanga, katika kukabiliana na changamoto hio, Wizara imefanya mapitio ya upembuzi yakinifu juu ya uingizaji wa madini ya ujenzi kutoka Tanzania Bara. Kupitia upembuzi huo tayari Wizara imeingia mkataba wa kuingiza mchanga kutoka Tanzania Bara na Kampuni mbili kwa ajili ya matumizi ya miradi ya kimkakati. Hatua hiyo itapunguza matumizi ya mchanga hapa nchini.

68. **Mheshimiwa Spika,** uchimbaji wa Maliasili Zisizorejesheka kwa upande mwengine husababisha uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, uhuishaji wa maeneo hayo baada ya kukamilika kwa uchimbaji hupunguza athari za uchimbaji huo kwa kiasi kikubwa na kusaidia ardhi kurudi katika hali yake ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2026 Wizara imehuwisha maeneo mawili (2) yenye ukubwa wa ekari 36, kupitia Taasisi ya EEEDO (Enviromental and Economic Empowerment Development Organnization) ambapo jumla ya miti 4,744 imepandwa..

69. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa changamoto zinazojitokeza katika usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka ni: -

i. Kuendelea kwa uchimbaji haramu wa maliasili zisizorejesheka, hususan mchanga, katika Mkoa wa Kaskazini Unguja licha ya juhudi zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto hii;

ii. Kuongezeka kwa utitiri wa machimbo ya vifusi katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar ambayo baadhi yao yanatokana na ujenzi wa miradi ya Barabara;

iii. Kuongezeka kwa kasi usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka nje ya muda ulioruhusiwa kisheria hasa nyakati za usiku;

iv. Kutofuata taratibu za usafirishaji ikiwemo kutokuwa na leseni ya ruhusa ya kusafirisha maliasili zisizorejesheka, kupakia kupita kiwango cha ujazo kilichoruhusiwa, kutokusimama katika vituo vya ukaguzi vya maliasili zisizorejesheka na kutofunika hali inayopelekea uharibifu wa barabara pamoja na kuathiri watumiaji wengine wa barabara; na

v. Baadhi ya gari zinazotumika katika utekelezaji wa miradi ya barabara zinauza kifusi kwa wananchi hali inayopelekea kuzorota kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia Wizara.

70. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua za kukabiliana nazo kama ifuatavyo: -

i. Wizara kwa kushirikiana na Vikosi vya ulinzi imekua ikifanya doria katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar pamoja na kufanya vikao na Serikali za Wilaya na Mkoa husika.

ii. Wizara imefanya vikao na Taasisi husika na kuwasisitiza kufuata utaratibu ikiwemo kutochimba maeneo mapya na badala yake kutumia maeneo yaliochimbwa zamani.

iii. Wizara imeziandikia barua Taasisi zinazotekeleza miradi ya Serikali kuzitaka kuzingatia taratibu za usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka ikiwemo kupima gari husika na kuacha kuuza maliasili hizo kwa wananchi badala ya kutumia kwa ujenzi wa miradi.

*Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM*

71. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Afisi Kuu - Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, programu hii iliidhinishwa kutumia jumla ya **TZS. 3.30 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara. Kati ya fedha hizo **TZS 1.57 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 1.72 bilioni** kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2026, programu hii imetumia jumla ya **TZS 2.28 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara. Kati ya fedha hizo **TZS 604.06 milioni** sawa na asilimia 38 kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 1.67 bilioni** sawa na asilimia 98 kwa ajili ya mishahara.

*Idara ya Uendeshaji na Utumishi*

72. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi pamoja na kuhakikisha stahiki za wafanyakazi zinapatikana kwa wakati. Wizara imeendelea na hatua za kuimarisha mazingira ya kazi na wafanyakazi pamoja kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Miongoni mwa stahiki hizo ni mishahara, malipo ya kujikimu na malazi, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, likizo na kusimamia shughuli zote za Uendeshaji wa Ofisi.

73. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi, 2025/2026, jumla ya wafanyakazi 122 wamelipwa mishahara pamoja na kulipiwa michango ya ZSSF na ZHSF. Aidha, wafanyakazi 18 wamepatiwa likizo ya kawaida na kulipwa stahiki zao za likizo. Vile vile, Wizara imefanikiwa kuratibu na kusimamia mafunzo kwa watumishi; jumla ya wafanyakazi 10 wamepatiwa ada ya mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 11 wamelipiwa ada ya mafunzo ya muda mfupi. Wafanyakazi 115 wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uelewa juu ya athari za rushwa na uhujumu wa uchumi pamoja na uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma na maadili ya kazi.

74. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufanya tathmini ya kazi kwa wafanyakazi wake kama taratibu na miongozo inavyoelekeza, jumla ya wafanyakazi 38 wamefanyiwa Tathmini ya Utendaji kazi na wafanyakazi 11 wamepandishwa Daraja kwa mujibu wa Miongozo ya Utumishi. Katika kuongeza Rasilimali watu, Wizara imepata Kibali cha Ajira kwa nafasi sita (6) na mchakato wa ajira hizo umekamilika kupitia Wizara husika.

75. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu na kusimamia Vikao mbali mbali ikiwemo; Vikao viwili (2) vya Kamati ya Uongozi, vikao vitatu (3) vya Kamati Tendaji, vikao viwili (2) vya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu wa Awali na Endelevu, vikao tisa (9) vya Bodi ya Zabuni pamoja na mambo mengine vikao vimejadili Mpango wa Manunuzi wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, kujadili ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2024/2025 na Mpango kazi wa ukaguzi Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kikao kimoja cha watumishi.

76. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufanya manunuzi ya vitendea kazi, kulipia huduma za uendeshaji wa Ofisi pamoja na usimamizi wa matengenezo ya vyombo vya usafiri. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu na kuuwasilisha Afisi Kuu ya Utumishi kwa hatua zinazofuata.

***Idara ya Mipango, Sera na Utafiti***

77. **Mheshimiwa Spika**, Idara hii ina jukumu la kuandaa, kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mipango, mikakati, programu na miradi iliyochini ya Wizara.

78. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza maandalizi ya Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Kwa sasa, inaendelea kufanya uchambuzi wa hali halisi kuhusu masuala ya sheria ya maji na kuandaa mapendekezo ya msingi. Baada ya hatua hiyo, rasimu ya sheria itaandaliwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa Water-IPF.

**79. Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara kupitia Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Nishati na Ufikiwaji wa Huduma ya Umeme Zanzibar (ZESTA) inaendelea kuandaa Sheria ya Nishati kwa kushirikiana na Mtaalamu Elekezi, kufuatia uzinduzi wa Sera ya Nishati ya Mwaka, 2025. Sambamba na hilo, inakamilisha Sera ya Madini kwa kuzingatia maoni ya Kamati ya Makatibu Wakuu. Hatua hizi zote zinalenga kuimarisha mfumo thabiti wa kisera na kisheria.

**80. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha kuandaa Mpango wa Kudhibiti Vihatarishi *(Risk Management Framework)* kama sehemu ya kuimarisha usimamizi wa vihatarishi katika utekelezaji wa majukumu yake. Mpango huo tayari umewasilishwa, na kwa sasa Wizara inaendelea na maandalizi ya Daftari la Vihatarishi *(Risk Register)* ili kutambua na kufuatilia vihatarishi vinavyojitokeza katika shughuli za kila siku na kupatiwa suluhisho.

**81. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na watendaji wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeendelea kukusanya takwimu zinazozalishwa na Wizara na kuzitengenezea utaratibu wa kuzichapisha na kuandaa kitabu cha takwimu (Statistical Abstract). Matarajio ya Wizara ni kutoa kitabu cha takwimu za wizara mwishoni mwa kila mwaka wa fedha.

**82. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji Unguja na Pemba kwa kushirikiana na taasisi za Serikali, zikiwemo Tume ya Mipango Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango (Idara ya Bajeti) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kupitia ufuatiliaji huo, changamoto kama ucheleweshaji wa miradi na ucheleweshaji wa vibali vya mizigo bandarini hubainishwa na kushughulikiwa kwa wakati. Wizara pia inaendelea kufanya mawasiliano ya karibu na wakandarasi ili kuongeza kasi ya utekelezaji. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya ZPDB, huwasilisha taarifa za utekelezaji zinazoainisha hatua zilizofikiwa, changamoto na mafanikio, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa miradi.

**83. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuratibu ushirikiano wa kisekta kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, pamoja na kusimamia utekelezaji wa Hati za Makubaliano na Wizara za Maji, Wizara ya Madini na Wizara ya Nishati za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja

na taasisi zake. Kupitia ushirikiano huo, Wizara imeanza kunufaika kwa kubadilishana wataalamu, kushirikiana katika maandalizi na utekelezaji wa miradi, pamoja na kushiriki kwa pamoja katika vikao vya kitaifa na kimataifa.

### *AFISI KUU - PEMBA*

**84. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini Pemba ina vitengo vinne (4) ambavyo ni Mipango, Sera na Utafiti, Uendeshaji na Utumishi, Nishati na Madini Maendeleo ya Maji na Taasisi tatu (3) ambazo ni ZAWA/Rand Water, ZECO na ZURA. Katika kipindi cha Julai –Machi 2025/2026, Afisi Kuu - Pemba imefanikiwa kutekeleza majukumu mbali mbali ikiwemo kuratibu vikao vitatu (3) vya wafanyakazi kwa ajili ya kusikiliza na kushughulikia changamoto zao, ambapo maamuzi yalifanyika na kutekelezwa kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi wa umma.

Aidha, vikao vitano (5) vya wafanyakazi wa Wizara vilifanyika vikilenga masuala ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, utambulisho wa viongozi, maandalizi ya ugeni na utekelezaji wa miradi. Vile vile, vikao viwili (2) vya Vitengo ya Nishati na Madini viliratibiwa kwa wafanyakazi wa vituo vya ukaguzi na madereva wanaoshughulikia usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka.

**85. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza ufanisi wa kazi, Afisi kuu Pemba inaendelea kusimamia sheria na kanuni za utumishi wa umma pamoja na maslahi ya wafanyakazi kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia mafunzo wafanayakazi watatu yanayohusu udhibiti na utunzaji wa taarifa. Aidha, wafanyakazi 33 walipatiwa mafunzo ya Mfumo wa Utunzaji wa Nyaraka *(e-office)* pamoja na mafunzo elekezi kutoka Idara na Vitengo tofauti.

**86. Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu -Pemba imewapatia mafunzo wananchi 33 kuhusu usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka (mawe, kokoto, mchanga, matofali ya mawe, fusi na vumbi) katika maeneo yao, ili kuendeleza sera na mfumo wa kisheria unaohusiana na masuala ya Nishati na Madini.

**87. Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu-Pemba kupitia Kitengo cha Mipango, Sera na Utafiti imeendelea kufuatilia miradi ya maji na umeme. Aidha, Timu ya Ufuatiliaji na Tathmini ilitembelea maeneo ya uchukuaji wa Maliasili Zisizorejesheka kupitia kitengo cha Nishati na Madini. Matokeo ya ufuatiliaji yalibaini uwepo wa utekelezaji mzuri wa miradi hiyo. Hali inayopelekea miradi kukamilika kwa wakati na kwa ufanisi.

**88. Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu Pemba kupitia Kitengo cha maendeleo ya Maji mnamo tarehe 29/08/2025 ilishiriki kikao kilichojumuisha *Rand Water* Pemba na Mradi wa UNICEF pamoja na Wadau wa Maji, Vyuo Vikuu, Halmashauri na Mabaraza ya Miji Wete, Chake Chake, Mkoani na Micheweni. kikao kilihusu kutunza vyanzo vya Maji Zanzibar na tafiti juu ya Maji safi na Maji taka.

**89. Mheshimiwa Spika,** kikao hicho kilizungumzia masuala ya utunzaji wa vyanzo vya maji kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya Tabia za nchi, upandaji miti katika vyanzo vya maji kwa kuweka viguzo na mabango pamoja na uchunguzi wa ubora wa maji katika visima binafsi. Kwa upande wa Pemba kazi hiyo imetekelezwa kwa ufanisi kama ilivyopangwa.

**90. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Afisi Kuu Pemba inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo; uhaba wa fedha za matumizi ya uendeshaji wa shughuli za ofisi, ufinyu wa ofisi na upungufu wa vyombo vya usafiri. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Afisi Kuu imeendelea kufanya mazungumzo kati ya Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili kuboresha upatikanaji wa fedha; imewasilisha mahitaji ya upatikanaji wa ofisi Wizarani; na kuwasilisha pia mahitaji ya vitendea kazi, ikiwemo vyombo vya usafiri, kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa kazi.

## C. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2025/2026

**91. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini (WMNM) inasimamia Taasisi tatu (3) zinazojitegemea na zilizoanzishwa kisheria ambazo ni: -

*i)* ***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA),*** ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya ZURA Na. 7 ya mwaka 2013, yenye jukumu la msingi la kudhibiti huduma za maji, nishati, gesi, mafuta na umeme kwa ajili ya kulinda watoa huduma na wapokea huduma.

*ii)* ***Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA),*** iliyoanzishwa kwa Sheria ya Maji Na. 4 ya mwaka 2006 yenye jukumu la kusimamia upatikanaji wa huduma za maji safi, salama na zenye ubora kwa wananchi wote wa Zanzibar. Aidha, katika kuimarisha utendaji wa majukumu yake, majukumu ya Mamlaka hii yamekasimiwa kwenda kwa Kampuni binafsi ya *Rand Water* Zanzibar yenye dhamana ya kuimarisha uendeshaji na usimamizi wa utekelezaji katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama.

*iii)* ***Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO),*** lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya ZECO Na. 3 ya mwaka 2006. Shirika hili lina mamlaka ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa umeme, pamoja na ununuzi wa umeme kutoka vyanzo mbali mbali hadi kuwafikia wateja.

### *a) Mamlaka ya Maji Zanzibar - Rand Water Zanzibar*

**92. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Maji Zanzibar kupitia Kampuni ya *Rand Water Zanzibar* ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS. 13.28 bilioni** zinazotokana na mauzo ya maji, ruzuku ya mshahara na mapato mengineyo. kati ya hizo **TZS. 10.11 bilioni** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara na **TZS. 3.17 bilion**i kwa ajili ya mauzo ya maji na mapato mengineyo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 *Rand Water* imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 9.10 bilioni** sawa na asilimia **68.40** ya makadirio ya mwaka na wastani wa asilimia **84.61** ya makadirio

ya kipindi cha miezi tisa. kati ya makusanyo hayo, **TZS. 2.37 bilioni** zilizotokana na mauzo ya maji na mapato mengineyo na **TZS. 6.72 bilioni** ni ruzuku ya mshahara.

**93. Mheshimiwa Spika,** *Rand Water Zanzibar* imepata mafanikio yanaonesha wazi mabadiliko halisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Rand Water imeendelea kuimarisha mtandao wa usambazaji wa maji ambapo jumla ya mivujo 976 ya mabomba yamerekebishwa na kuzibwa kwa Unguja na Pemba. Hatua hii imepunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa maji na wakati huo huo kuboresha kasi ya maji katika maeneo mengi, hivyo kufanya huduma hii kuwa ya uhakika zaidi kwa wananchi. Hatua hii imeongeza upatikanaji wa maji, kupunguza malalamiko ya wananchi na kuokoa rasilimali maji ambayo awali ilikuwa ikipotea ardhini.

**94. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, *Rand Water* imefanikiwa kuongeza upatikanaji wa pampu ambapo kiwango hiki kimetokana na maboresho ya kiufundi na kupunguza muda wa matengenezo. Hali hii imeboresha mifumo ya uzalishaji wa maji na upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Aidha, Serikali kupitia Rand Water Zanzibar imeendelea na uimarishaji wa miundombinu muhimu kwa mfano Visima vya kituo cha Kidutani chenye tangi kubwa la ujazo wa lita 32.5 milioni vimeboreshwa. Mafanikio haya yameongeza uwezo wa uzalishaji, uhifadhi wa maji na kuboresha huduma hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

**95. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha uzalishaji wa maji ya visima, *Rand Water* imefanikiwa kufufua, kusafisha na kukarabati visima 28, hatua iliyorejesha uwezo wake wa uzalishaji na kupunguza athari za mchanga ambazo zilikuwa zikichangia kupungua kwa ufanisi wa visima hivyo. Sambamba na hilo, maabara za maji za Unguja na Pemba zimeboreshwa kwa kuwekwa vifaa na taratibu za uendeshaji kitaalamu (SOPs), hatua inayohakikisha ubora wa maji unaozalishwa na kusambazwa kwa wananchi unafikia viwango vinavyokubalika.

**96. Mheshimiwa Spika,** *Rand Water* imeendelea kufanya ukaguzi wa mifumo ya umeme na kuimarisha vifaa vya umeme katika vibanda vya

kuhifadhia pampu. Baadhi ya vifaa vya umeme katika vibanda vya pampu vilikarabatiwa ili kuhakikisha uzalishaji wa maji unaendelea bila kukatika mara kwa mara. Hata hivyo, changamoto za umeme na wizi wa nyaya bado zinaathiri ufanisi wa kazi hizi.

**97. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha usalama wa afya ya wananchi, Rand Water Zanzibar imekamilisha jumla ya mizunguko 12 ya ufuatiliaji wa ubora wa maji, ambapo sasa ukusanyaji wa takwimu umeboreshwa kutoka mfumo wa miezi sita hadi kufanyika kila mwezi. Hii ni hatua kubwa inayoiwezesha Serikali kuchukua hatua za haraka pale changamoto zinapojitokeza na hivyo kulinda afya za wananchi kwa ufanisi zaidi.

**98. Mheshimiwa Spika,** Rand Water Zanzibar pia imeanza matumizi ya teknolojia ya mita za kisasa kwa majaribio, hatua inayolenga kuboresha ukusanyaji wa mapato, kuongeza uwazi na kusaidia upangaji bora wa matumizi ya maji. Wakati huo huo, jitihada zimefanyika katika kuimarisha ulinzi wa miundombinu ya maji, hususan katika visima vilivyokuwa hatarini, ambapo hatua za kiusalama zimechukuliwa ili kupunguza matukio ya wizi na uharibifu.

**99. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Rand Water Zanzibar imeendelea kuweka kipaumbele katika sekta ya afya na Usafi wa Mazingira (WASH) kwa kuhakikisha huduma ya maji inaimarishwa katika hospitali za Chumbuni, Kivunge na Mbuzini. Hatua hii inalenga kuhakikisha huduma za afya zinatolewa katika mazingira salama na yenye uhakika wa maji safi na salama. Vile vile, juhudi za kuzuia uchafuzi wa maji zimeimarishwa kupitia uwekaji wa vifuniko maalum na ulinzi wa visima, hatua inayolinda rasilimali hii muhimu dhidi ya athari za mazingira na shughuli za kibinadamu.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika eneo la usimamizi wa fedha, Rand Water Zanzibar imeendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha na kuhakikisha kufungwa kwa hesabu kwa wakati na kupata matokeo mazuri ya awali ya ukaguzi. Hata hivyo, bado kuna changamoto katika ukusanyaji wa mapato na madeni, ambazo Serikali inaendelea kuzifanyia kazi kwa lengo la kuhakikisha uendelevu wa kifedha wa sekta hii muhimu.

101. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, mafanikio haya yanaonesha wazi kuwa juhudi za Serikali zinaendelea kuleta matunda na kwamba hatua zinazochukuliwa zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi. Haya ni mafanikio ya vitendo, yanayoonekana na yanayoleta matumaini mapya katika Sekta ya Maji kwa wananchi wa Zanzibar.

102. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uharibifu wa mabomba wakati wa ujenzi wa barabara unaosababisha upotevu wa maji na ongezeko la gharama za ukarabati; uhaba wa magari ya kazi na vifaa unaochelewesha matengenezo ya dharura pamoja na upungufu wa vifaa vya usalama (PPE); mifumo chakavu ya kutibu maji, uhaba wa kemikali za maabara, uchache wa wafanyakazi wenye weledi na uzalendo, vifaa vya mita; upotevu mkubwa wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu hasa mabomba ya Asbestos na PVC; pamoja na uvamizi na hujuma katika vyanzo vya maji.

103. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hizo, Taasisi imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kufunga vifaa vya kudhibiti umeme kulinda pampu, kubadilisha mabomba chakavu ili kuimarisha huduma ya maji, kulinda vyanzo vya maji kwa kujenga uzio na kuimarisha ulinzi, pamoja na kuwasiliana na Wizara ya Miundombinu kwa ajili ya urejeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya maji.

### *b) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)*

104. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS. 265.32 bilioni** kutokana na mauzo ya umeme na mapato mengineyo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 ZECO imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 175.65 bilioni,** sawa na asilimia **66.20** ya makadirio ya mwaka na wastani wa asilimia **103** ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa. Kati ya makusanyo hayo, **TZS. 136.90 bilioni** zimetokana na mauzo ya umeme, **TZS. 23.11 bilion**i mapato mengineyo na **TZS. 15.64 bilioni** ni makusanyo ya madeni. Aidha, ZECO imetumia jumla ya **TZS. 180.48 bilioni** kwa kazi za maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo.

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi hadi Machi, 2026 Shirika la Umeme limepanga kutumia **TZS. 14.33 bilioni** kwa kazi ya usambazaji wa huduma ya umeme Shirika la Umeme limepanga kufanya usambazaji wa huduma ya umeme katika vijiji 45, (27 Unguja na 18 Pemba). Hadi sasa, huduma ya umeme imepelekwa katika vijiji 31 (23 Unguja na 8 Pemba) kwa gharama ya **TZS. 2.402 bilioni**. Kiambatisho Namba 3 kinahusika.

106. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi 2025/2026, Shirika la Umeme limepanga kutumia **TZS. Bilioni 12.28** kwa kazi ya usambazaji wa huduma ya umeme katika vijiji 22, ambapo Unguja 14 na Pemba nane (8). Kwenye utekelezaji wa kazi hiyo, ZECO imepeleka huduma ya umeme katika vijiji 20 ambapo Unguja 13 na Pemba saba (7) vilivyogharimu jumla ya **TZS. 1.59 bilioni** sawa na asilimia 91 ya vijiji vyote vilivyopangwa.

107. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Shirika la Umeme lilipanga kutumia **TZS 1.36 bilioni** kwa utekelezaji wa kazi za uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu ya umeme. Kazi zilizofanywa katika uimarishaji na uendeshaji wa miundombinu ya umeme ni: -

i. Kusawazisha maeneo yenye umeme mdogo. Katika kazi hii, Shirika limefanikiwa kuimarisha upatikanaji wa kiwango kizuri cha umeme katika jumla ya maeneo 23 (Unguja 21 na Pemba mbili (2) yaliyokuwa yakikabiliwa na changamoto ya umeme mdogo. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 106 ya mpango uliowekwa wa kurekebisha umeme mdogo katika maeneo 22 (Unguja 18 na Pemba nne (4) ***Kiambatisho Namba 4***.

ii. Shirika la Umeme limefanikiwa kuwaunganishia huduma ya umeme jumla ya wateja wapya 20,337 (18,490 Unguja na 1,847 Pemba), ambapo ni sawa na asilimia 105 ya wateja 19,398 (Unguja 15,798 na Pemba 3,600) waliopangwa kuunganishiwa umeme katika kipindi hicho.

iii. Kubadilisha nguzo mbovu, Shirika limefanikiwa kubadilisha jumla ya nguzo mbovu 1,140 (652 Unguja na 488 Pemba).

iv. Shirika limefanikiwa kufanya ukaguzi wa jumla ya transfoma 497 (Unguja 209 na Pemba 288). Ukaguzi huo ni sawa na asilimia 67 ya

transfoma 740 (500 Unguja na Pemba 240) zilizopangwa kukaguliwa katika kipindi hicho. Kati ya transfoma 497 zilizokaguliwa, jumla ya transfoma 22 kwa Unguja na 18 kwa upande wa Pemba zilibainika kuwa na hitilafu na kufanyiwa masawazisho stahiki.

***Hali ya Madeni ya Wateja wa ZECO***

108. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Shirika la Umeme Zanzibar limekuwa likikabiliana na changamoto mbali mbali ikiwemo changamoto ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja wake, uwepo wa malimbikizo ya madeni kwa wateja wa Shirika la Umeme unatokana na baadhi ya wateja kushindwa kulipa ankara zao za matumizi ya umeme kwa ukamilifu na wakati. Hali hiyo inatokana na utaratibu usioepukika wa matumizi ya umeme kabla ya malipo kwa baadhi ya Taasisi ambazo bado zoezi linaloendelea la ufungaji wa "Pre-paid Meters" kwa wateja wakubwa halijawafikia.

109. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026, Shirika linawadai wateja wake jumla ya **TZS. 53.15 bilioni** ambapo mchanganuo wake unaonekana katika Jadweli lifuatalo.

Jadweli: linaonesha mchanganuo wa madeni ya umeme Unguja na Pemba hadi Machi 2026

| **MUHTASARI WA MADENI** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na** | **JINA LA TAASISI** | **DENI (UNGUJA)** | **DENI (PEMBA)** | **JUMLA YA DENI UNGUJA NA PEMBA** |
| 1 | ZAWA | 21,509,200,375.95 | 8,666,820,436.09 | 30,176,020,812.04 |
| 2 | TAASISI BINAFSI | 6,792,511,556.52 | - | 6,792,511,556.52 |
| 3 | TAASISI ZA SERIKALI | 14,684,299,255.02 | 1,501,625,839.09 | 16,185,925,094.11 |
| **JUMLA** | | **42,986,011,187.49** | **10,168,446,275.18** | **53,154,457,462.67** |

110. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Taasisi za Serikali (SMZ na SMT), Shirika limekuwa likifanya juhudi za kufanya vikao mbali mbali na Viongozi wa Taasisi hizo lakini bado baadhi ya Taassi zimekua na muitiko mdogo wa kufanya malipo yake ipasavyo na kulikosesha Shirika mapato yake stahiki.

### c) *Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)*

111. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS. 31.16 bilion**i kutokana na tozo la Mamlaka Regulatory Levy inayotokana na mafuta, gesi ya kupikia (LPG) mapato ya leseni na mapato mengineyo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 ZURA imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 23.69 bilioni**, sawa na asilimia 76.03 ya makadirio ya mwaka na wastani wa asilimia **95** ya makadirio ya kipindi cha tathmini. Kati ya makusanyo hayo, **TZS. 23.38 bilion**i zimetokana na tozo za huduma na **TZS. 318.9 milioni** ni mapato mengineyo. Aidha, ZURA imetumia jumla ya **TZS. 27.35 bilioni** kwa kazi za maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo na mchango wa Serikali.

112. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na matumizi yaliyotajwa hapo juu, Mamlaka ilipokea na kutumia jumla ya TZS. 50.00 bilioni kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Fedha hizi zilikuwa mkopo mahsusi kwa ajili ya kulipa deni la Kampuni ya Uletaji Mafuta nchini, deni lililotokana na gharama za ubadilishaji wa fedha za kigeni. Hatua hii pia ililenga kupunguza athari za kupanda kwa bei za mafuta kwa wananchi, hasa katika kipindi ambacho kulitokea upungufu wa dola za Kimarekani sokoni kutokana na vita kati ya Urusi na Ukraine. Hivyo basi, jumla ya matumizi yaliyofanyika katika kipindi cha miezi tisa (9) **TZS. 77.36 bilioni.**

113. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imepitia Miongozo ya Usimamizi na Utoaji wa Huduma za Maji, kutafsiri Kanuni ya Kusimamia Huduma za Ubora wa Maji ya mwaka 2026 na kufanya mapitio ya Muongozo wa Ubora wa Maji ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa sekta katika eneo la maji. Aidha, imeandaa rasimu ya Kanuni ya Umeme ya Gridi Ndogo ya Mwaka 2025, kufanya mapitio ya vielelezo vya PPA vinavyohusiana na jua, upepo, gesi na mafuta, kutafsiri rasimu za Kanuni ya Umeme ya Gridi Ndogo na Kanuni ya Usimamizi wa Mikataba ya Ununuzi wa Umeme pamoja na kupitia na kutafsiri Kanuni ya Vilainishi vya Petroli ya Mwaka, 2026.

114. **Mheshimiwa Spika,** aidha, ZURA imepitia Muongozo wa Ukaguzi, imeandaa rasimu ya awali ya mikataba ya upimaji wa utekelezaji, pamoja na kufanya maboresho ya mfumo wa ZIRS. ZURA pia imeboresha mfumo wa ERMS kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGAZ), imefanya mapitio na kuandaa Muongozo wa mafunzo na Mpango wa Urithishaji, imefanya mapitio na kutafsiri miongozo na Sera za Rasilimali watu pamoja na kuandaa Mpango wa Rasilimali Watu wa Miaka Mitano. Haya yote ni miongoni mwa maagizo ya Serikali ya kutaka kufanya mapitio ya Sheria, Sera na kununi ambazo zitaleta ufanisi katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu.

115. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea na shughuli za ukaguzi wa ubora wa maji yanayosambazwa kwa watumiaji katika baadhi ya vyanzo na miundombinu ya maji kwa Wilaya za Unguja na Pemba. Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za maji pamoja na usalama wa vyanzo vinavyotumika kuzalisha maji Mamlaka imefanya ukaguzi wa miundombinu ya maji Mkoa wa Kusini Unguja katika Wilaya za Kusini, Wilaya ya Kati, wilaya ya Kaskazini ‘A’, Kaskazini ‘B’ na Wilaya ya Magharibi B. Jumla ya vyanzo vya maji 123 vinavyotumika kuzalisha maji pamoja na miundombinu yake vimekaguliwa kwa kuangaliwa marekebisho yaliyotakiwa kufanywa kutoka kaguzi za nyuma (Compliance monitoring) pamoja na kaguzi za kawaida (routine monitoring) katika wilaya hizo. **Jadweli Namba 1 linahusika**.

116. **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi uliofanyika umebaini changamoto kadhaa katika maeneo mbalimbali ya visima na miundombinu ya maji. Baadhi ya visima havina uzio na vimevamiwa, kanuni za usalama hazijabandikwa, na takwimu za uzalishaji hazipo sawa kutokana na hitilafu za flow meters na mfumo wa HMI. Aidha, mazingira ya visima yamezungukwa na majani, kuna changamoto za umeme na transfoma na visima kadhaa havifanyi kazi katika wilaya za Kaskazini ‘A’ na ‘B’. Vilevile, baadhi ya surface pumps na mitambo ya kutibu maji haifanyi kazi ipasavyo, hali ambayo imeathiri uzalishaji na usambazaji wa huduma za maji. Mdhibiti ameagiza hatua za haraka ikiwemo: kujenga uzio imara, kuandaa na kubandika kanuni za usalama, kurekebisha flow meters na HMI, kusafisha maeneo ya visima

mara kwa mara, kuboresha miundombinu, kufanya matengenezo ya pumps na mitambo ya maji, pamoja na kuandaa mpango wa dharura na wa muda mrefu wa kuboresha huduma za maji.

117. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imeendelea kukagua ubora wa maji yanayowafikia wananchi katika vyanzo na miundombinu ya maji inayotoa huduma katika maeneo tofauti. Zoezi hili lilijumuisha upimaji wa tabia za maji katika nyanja za *physiochemical parameters* ikijumuisha *Electrical Conductivity (EC), Total Dissolved Solid (TDS), pH, Temperature na Residual Chlorine.*

118. **Mheshimiwa Spika,** kiujumla matokeo yameonesha kuwa ubora wa maji umekidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) kupitia *Zanzibar Standards, Drinking (potable) water (ZNS 57: 2015) specification*. Aidha, baadhi ya visima ambavyo viwango vyake vya chumvi kwa kiashiria cha Electrical Conductivity (EC) huvuka 1000 µS/cm zoezi maalumu la ufuatiliaji na upimaji limeendelea kufanyika na kuweka mlinganisho wa taarifa zake za mwaka wa fedha uliopita ambazo husaidia kufahamu mwenendo wa vyanzo hivi.

119. **Mheshimiwa Spika,** kiujumla matokeo ya ukaguzi wa visima na vyanzo hivi vimeonesha baadhi ya vyanzo viwango vyake vya chumvi kuongezeka kutoka Julai 2025 hadi Machi 2026, kwa mfano maeneo ya Jambiani Kibigija, Muyuni na Ukongoroni na kwa kisima cha Unguja Ukuu, Mtende na Kisongoni vimeonekana kupungua kidogo kwa kiwango cha chumvi.

120. **Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi wa uwekaji wa dawa ya Residual Chlorine katika maeneo ya kuhifadhi maji na vituo vya wateja, matokeo yanaonyesha kwa kiwango kikubwa skimu zilizopimwa zipo katika hali ya kuridhisha, zikifuata viwango vinavyopendekezwa na WHO na TBS (0.2–0.5 mg/L kwa mtandao wa usambazaji na 0.8–1 mg/L kwa contact tanks). Hata hivyo, baadhi ya vituo vya Mfenesini, Mangapwani, Sea Cliff, Chuini na Mbuzini vilionekana kuwa vipo vya chini ya kiwango ambapo kwa sasa hatua za marekebisho hayo zinaendelea.

121. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ofisi ya ZURA Pemba ilikagua miundombinu ya maji, katika Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba jumla ya visima 126. Visima 70 vimekaguliwa katika Mkoa wa Kusini, visima 30 katika Wilaya ya Mkoani na 40 katika Wilaya ya Chake Chake. Aidha, visima 56 vimekaguliwa Mkoa wa Kaskazini ambapo visima 32 katika Wilaya ya Wete na 24 katika Wilaya ya Micheweni.

122. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya ukaguzi katika Mkoa wa Kusini na Kaskazini yamebainisha changamoto zinazohusiana na visima vya maji, zikiwemo visima ambavyo havifanyi kazi, visima vyenye uzio mbovu, visima visivyo na uzio, visima vyenye mifuniko isiyo rasmi pamoja na baadhi ya wellhead zimebainika kuvujisha. ZURA iliwasilisha ripoti hii kwa mtoa huduma na kujadili hatua za kuchukuliwa.

123. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kupitia Ofisi ya ZURA Pemba ilikagua miundombinu ya umeme Tanga ili kutathmini matumizi, kumbukumbu za kukatika kwa huduma na hali ya nguzo katika njia ya kusafirisha umeme kutoka Majani Mapana hadi Mnyanjani. Jumla ya nguzo 113 zimekaguliwa na kubainika mapungufu ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

124. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa udhibiti umeme na usimamizi wa upatikanaji bora, endelevu na salama wa huduma za Nishati, ZURA kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) imefanya ukaguzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuchagua maeneo tofauti ya njia za kusambazia umeme kwa lengo la kutambua hali halisi ya miundombinu na huduma inayotolewa kwa wananchi, ambapo jumla vituo 155 vimekaguliwa katika mtandao wa Shirika la Umeme. Matokeo ya ukaguzi huo yalibaini mambo mbali mbali kama ifuatavyo:-

***1) Udhibiti wa Transfoma - Transfoma ya Paje Duarani 2000kVA***

125. **Mheshimiwa Spika,** transfoma imekingwa kwa kutumia fyuzi za (drop out fuses) ambapo kwa mujibu wa ukubwa wa tranfoma ya 2000kVA inatakiwa kuwekewa vifaa vya usalama vya kuilinda, ili transfoma hii iwe kituo kinachojitegemea katika uendeshaji wake.

2) *Uwekaji wa Fyuzi (HT and LT Fuses)*

126. **Mheshimiwa Spika,** Transfoma 24 kati ya 101 zilizokaguliwa katika Mkoa wa Kusini zimebainika kuwa na kasoro za kiufundi katika kifaa cha kudhibiti usalama wa transfoma na watumiaji kwa kufungwa isivyo sahihi kwa kutumia fyuzi waya bila ya jumba (fuse holder) kwa upande wa umeme mkubwa na kwa umeme mdogo zimefungwa moja kwa moja (direct connections). kwa kutumia kiungio (T off). Baadhi ya Transfoma hizo ni Tunguu Chuo Ndani, Bwejuu Skuli, Ndagaa Njia Panda na Mchangani Shamba.

*3) Nguzo za kuzuilia Transfoma*

127. **Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi, kumebainika kuwepo kwa vituo sita (6) vya transfoma ambavyo nguzo za kuzuilia zimeoza na zinaweza kusababisha uharibifu wa kifaa na kukosekana kwa huduma ya umeme, miongoni mwa vituo hivyo ni transfoma ya Tunguu Chuo Ndani, Kibele Zenj Water, Muyuni Skuli na Ghana Skuli.

*4) Kuharibika kwa Vidhibiti Radi*

128. **Mheshimiwa Spika,** vituo saba (7) vya transfoma katika sehemu zilizowekwa kifaa cha kulinda na kuthibiti radi isiunguze transfoma, kifaa hicho cha kudhibiti radi (lightning arrester) vimeharibika kwa kukatika. Miongoni wa Vituo vya transfoma hizo ni Ghana Skuli, Paje Makaburini, Makunduchi Cottage, Jambiani Gym na Manyame.

*5) Kuvuja kwa Mafuta ya Transfoma*

129. **Mheshimiwa Spika**, transfoma tano (5) zimegundulika kuvujisha mafuta kutokana kuzidi kwa matumizi ukilinganisha na uwezo wa transfoma au kutokufanyiwa matengenezo ya kinga kwa wakati. Hivyo, kuendelea kuvuja mafuta ya transfoma kutapelekea kuharibika kwa transfoma na kukosekana kwa huduma ya umeme kwa wananchi. Vituo vya transfoma hizo ni Makunduchi Cottage, Makunduchi Njia ya Vigaeni, Makunduchi Vigaeni Mwisho, Mchangani Shamba na Njia ya Cheju.

*6) Mpangilio Hafifu wa Waya za Transfoma*

130. **Mheshimiwa Spika,** baadhi ya vituo vya kusambazia umeme vina miundombinu duni ya ufungaji wa waya (Transformer Dressing). Vituo hivyo ni kama kituo cha Makunduchi Cottage, Mwera Mishokishokini, Tunguu Chuoni Getini, Ndijani kwa Baniani na Ndijani Nyambiza.

*7) Ukaguzi wa Miundombinu ya Umeme Ras Kiromoni Dar es salaam*

131. **Mheshimiwa Spika,** ZURA kwa kushirikiana na ZECO ilikagua Kituo cha Kupozea Umeme Tegeta na mfumo wa kusafirisha umeme Ras Kiromoni na kubainika miundombinu iko salama, yenye ufanisi na ina uwezo wa kuendeleza upatikanaji wa umeme Zanzibar; mfumo huo unajumuisha waya wa zamani unaosafirisha hadi 40 MW kwa kutumia kimiminika cha mafuta na waya mpya wenye uwezo wa kusafirisha hadi 100 MW bila kutumia mafuta, na kwa ujumla uko katika hali nzuri.

132. **Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, katika ukaguzi huo imebainika kuwepo kwa baadhi ya vifaa vya kudhibiti vilivyohitaji kuboreshwa ili viendane na teknolojia za kisasa, eneo la kuhifadhi mafuta kutumika kama ghala la kuhifadhi vitu vingine ambavyo havihusiani na malengo yaliyokusudiwa na kuwepo kwa mapungufu katika Mfumo wa earthing yaliyohitaji kuimarishwa ili kuhakikisha usalama kamili wa mfumo wa umeme.

133. **Mheshimiwa Spika,** ZURA ilikagua miradi mitatu (3) ya uzalishaji wa umeme wa jua Zanzibar, ikiwemo mradi wa Bambi (Generation Capital) unaotarajiwa kuongeza MW 19.4 kwenye gridi ya taifa, mradi wa Baraza Resort & Spa wenye uwezo wa MW 1 uliokuwa unahitaji kuhuishwa leseni, pamoja na mfumo wa Rooftop Solar PV wa Hoteli ya Riu Swahili wenye uwezo wa kV 490, lengo la ukaguzi huo lilikuwa kufuatilia maendeleo ya miradi, kuhakikisha viwango vya kiufundi vinazingatiwa na kuimarisha upatikanaji wa nishati safi, ambapo mradi wa Bambi unatarajiwa kupunguza utegemezi wa umeme kutoka Tanzania Bara, kupunguza gharama za uendeshaji na kuchangia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

134. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imesimamia zoezi la usajili wa mafundi umeme ili kuongeza usalama katika miundombinu ya umeme na kuimarisha ulinzi kwa wateja na mafundi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma. Vile vile, kuongeza fursa za ajira kwa mafundi umeme na vijana wanaofanya kazi za fitting za umeme, kuwapatia mafunzo na mipango endelevu ya kusimamia vyema miundombinu ya umeme.

135. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya fomu za maombi 2,725 zilitolewa na fomu za maombi 2,242 zilirejeshwa sawa na asilimia 82 ya fomu zilizochukuliwa. Maombi hayo yalikuwa katika madaraja mbali mbali kama ifuatavyo: -

**Daraja A:** Ni mafundi ambao wanauwezo wakufanya kazi katika ngazi zote za umeme ikiwemo kazi maalumu ambapo jumla ya fomu za maombi 57 zimepokelewa.

**Daraja B:** Ni mafundi wanauwezo wakufanya kazi mpaka kwenye mkondo wa umeme wa 33kV ambapo jumla ya fomu za maombi 51 zimepokelewa.

**Daraja C:** Ni mafundi wanaouwezo wakufanya kazi katika mkondo wa umeme usiozidi 400V ambapo jumla ya fomu za maombi 1,951 zimepokelewa.

**Daraja D:** Ni mafundi ambao wanafanya kazi maalumu kama vile za kuunga umeme wa Jua, Majokofu na kazi nyengine ambapo jumla ya fomu za maombi 183 zimepokekewa.

136. **Mheshimiwa Spika,** mafundi waliomba vibali kwa ajili ya kujishughulisha na uunganishaji wa mifumo ya umeme ni 2,242 kwa Unguja na 317 kwa Pemba ambapo mafundi wote wanatarajiwa kufanyiwa tathmini ya awali kwa ajili ya kupatiwa vibali na kuingizwa katika kanzidata.

137. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilikadiria kuingiza mafuta lita 225,000,000 ambapo kiwango halisi cha mafuta yaliyoingizwa nchini yalifikia lita 242,763,148 ambayo sawa na asilimia 107.89 ya makadirio ya kipindi hicho. Kwa upande wa matumizi jumla ya lita 239,019,135 yaliweza kutumika. Kwa upande wa Pemba, ZURA ilisimamia zoezi la uingizaji na akiba ya mafuta ambapo jumla ya lita 22,352,003 ziliingizwa na jumla ya lita 21,766,972 zilitumika, mchanganuo wa kila aina ya mafuta ni kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Namba 5 kinahusika***.

**138. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kufanya ukaguzi wa Bohari saba (7), sita (6) kwa upande wa Unguja na moja (1) kwa Pemba pamoja na vituo vyote 127 vilikaguliwa, vituo 104 kwa Unguja na 23 kwa Pemba. Aidha, ZURA kwa kushirikiana na Taasisi nyengine za Serikali zilifanya ukaguzi wa maeneo 12 yanayotarajiwa kujengwa vituo vya mafuta na kutakiwa kukusanya nyaraka zinazohitajika, ili kupatiwa vibali vya ujenzi, maeneo hayo ni: Dimani, Fuoni, Gamba, Charawe, Chukwani Buyu, Paje, Fumba, Uroa, Bungi, Magereza, Makunduchi na Matemwe. ***Kiambatisho Namba 6 kinahusika.***

**139. Mheshimiwa Spika,** ZURA pia iliendelea kufanya ukaguzi wa bei za mafuta katika vituo ili kujiridhisha iwapo bei halisi zilizotangazwa ndizo zinazotumika. Ukaguzi umeonyesha vituo vyote viliweka bei elekezi zilizotangazwa na Mamlaka kwa upande wa Unguja na Pemba. ***Kiambatisho Namba 7 kinahusika.***

**140. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kusimamia uingizaji na matumizi ya Gesi ya Kupikia (LPG), Kampuni zinazoingiza na kuuza gesi kwa jumla katika visiwa vya Zanzibar ni nne (4), ambazo ni ORYX Gas ZNZ Ltd, Lake Gas Ltd, Taifa Gas ZNZ Ltd na Al Nabahan Gas Supply (O-Gas), kiwango cha Gesi kilichoingizwa nchini ni kilogramu 10,563,306 na kiwango cha matumizi kimefikia kilogramu 11,213,942. ***Kiambatisho Namba 8 kinahusika.***

**141. Mheshimiwa Spika,** kiutaratibu bei za Gesi hupangwa na kampuni zinazoingiza Gesi kwa ujumla na kuridhiwa na Mamlaka. Kwa upande wa Pemba Jumla ya kilogramu 503,484 za gesi ya kupikia zimeingizwa na wasambazaji wakuu ambao ni ZANZIGAS COMPANY LTD, TAIFA GAS na O-GAS; na kilogramu 522,098 zimetumika. Aidha, ZURA Pemba imefanya ukaguzi wa miundombinu ya gesi ya kupikia kwa wauzaji watatu (3) wa jumla ambao ni ZANZIGAS, SAMIS GAS na AL-MAULY GAS SUPPLY.

**142. Mheshimiwa Spika,** kufuatia matumizi ya gesi ya LPG katika vyombo vya moto, Mamlaka imepokea ombi kutoka kampuni ya Oryx Zanzibar la kujenga kituo cha kujazia gesi ya LPG (Autogas Station) katika eneo la Fuoni Petrol Station. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa eneo hilo

halikidhi viwango vinavyohitajika kwa ujenzi wa kituo hicho. Kwa msingi huo, mwombaji ameshauriwa kutafuta eneo mbadala au kituo kingine kinachokubaliana na masharti na viwango vya kisheria vilivyowekwa. Hatua hii inalenga kuhakikisha usalama, ufanisi na uendelevu wa huduma za gesi ya LPG kwa mujibu wa kanuni.

143. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha ZURA inaboresha uwezo wa Taasisi wa Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati, ilipitia Nyaraka za BPS (Review BPS Documents) na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mkataba kati ya OMCs na mletaji mafuta, kushiriki uzinduzi wa Tanzania Energy Association (TEA) pamoja na kuendelea kuwasimamia wafanyakazi katika mafunzo ya muda mrefu, Watumishi tisa (9) wanasomeshwa na Mamlaka na watumishi watatu (3) wamepata ufadhili kupitia vyuo Tofauti nje ya nchi, Wafanyakazi 19 wamepelekwa mafunzo ya muda mfupi ya usimamizi wa maji taka na mafunzo ya upatanishi na usuluhishi katika Chuo cha *Tanzania Institute of Arbitrators* (TIArb) Dare Es Salaam.

144. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Mamlaka iliendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na makongamano ya kijamii kwa ajili ya kujitangaza, pamoja na kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati. Katika kufanikisha hayo, Mamlaka iliendesha vipindi vya redio kuhusu Mafanikio ya ZURA, Matumizi salama ya Gesi ya kupikia na Usalama katika Vituo vya Mafuta.

145. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imeendelea kufanya Makongamano na kukutana na Waandishi wa Habari kwa ajili ya kutangaza bei za mafuta kwa kila mwezi pamoja na kutangaza taarifa hizo kupitia mitandao ya kijamii, imetoa Taarifa na (Posts) mbali mbali katika mitandao ya kijamii (Facebook na Instagram) na YouTube, imeshiriki katika Vikao Kazi vitatu (3); Kikao Kazi cha Maafisa Habari na Uhusiano, Kikao kazi cha Maafisa Huduma kwa Wateja na Kikao Kazi cha Maafisa Mawasiliano, Habari na Uhusiano.

146. **Mheshimiwa Spika,** ZURA pia imepokea na kufuatilia jumla ya malalamiko sita (6) ambayo yanahusu kuongezewa Bili za Umeme, malalamiko manne (4) kati ya hayo yameshatatuliwa na mawili (2) yapo katika hatua za uchunguzi na usuluhishi.

147. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imetambua ongezeko la bei za mafuta duniani linalosababishwa na migogoro ya kimataifa na athari zake kwa uchumi wa ndani. Ili kulinda ustawi wa wananchi, imetangaza bei elekezi ya **TZS. 3,500** kwa lita ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa mwezi Aprili 2026, sambamba na kutoa ruzuku inapobidi ili kuhakikisha gharama za nishati zinabaki himilivu na hazileti mzigo mkubwa kwa wananchi. Hatua hizi zinakusudia kupunguza shindikizo la mfumuko wa bei na kudhibiti gharama za maisha.

148. **Mheshimiwa Spika,** kwa muda wa kati na mrefu, Serikali imepanga kuanzisha hifadhi ya kimkakati ya mafuta ndani ya mwaka mmoja na kuharakisha uwekezaji katika nishati mbadala kama umeme wa jua na gesi asilia. Aidha, juhudi zitaelekezwa katika kuhamasisha matumizi bora ya nishati ili kupunguza gharama kwa watumiaji na kuimarisha udhibiti wa sekta ya nishati. Serikali imewahakikishia wananchi kuwa itaendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari za mabadiliko ya bei na kulinda maisha bora ya wananchi.

### *UTEKELEZAJI WA BAJETI INAYOZINGATIA JINSIA(GRB)*

149. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza bajeti inayozingatia jinsia kwa kuimarisha upatikanaji wa nishati safi, hususan kupikia, ili kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa ambao unaathiri zaidi wanawake. Kupitia miradi ya nishati, Serikali inalenga kuongeza matumizi ya LPG, majiko sanifu na nishati jadidifu, sambamba na utoaji wa ruzuku na elimu kwa jamii. Zaidi ya kaya 10,000 zinatarajiwa kunufaika, huku wanawake wakiwa walengwa wakuu. Aidha, wanawake wanawezeshwa kiuchumi kupitia ajira na ujasiriamali katika mnyororo wa thamani wa nishati safi, pamoja na kuongezewa ushiriki wao katika mafunzo ya kitaalamu na nafasi za kiufundi.

150. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama, ambapo huduma hii imefika katika maeneo mengi mjini na vijijini. Hatua hii imepunguza muda wa kutafuta maji, hasa kwa wanawake na watoto wa kike, na hivyo kuwawezesha kushiriki zaidi katika shughuli za kiuchumi na kijamii.Vile vile, miundombinu ya maji imeimarishwa

katika maeneo ya mijini na vijijini, huku wanawake wakihusishwa katika usimamizi wa rasilimali za maji kupitia kamati za jamii. Juhudi hizi zimechangia kuboresha afya, kupunguza pengo la kijinsia na kuimarisha ustawi wa wananchi kwa ujumla.

151. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia Sekta ya Maji na Nishati. Katika kipindi cha Julai -Machi, 2025/2026, miradi mbali mbali imetekelezwa kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Namba 9.***

## *D. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027*

152. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027 itatekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuimarisha na kuongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya ya Kati, hususan katika maeneo yaliyotekelezwa na miradi mbalimbali, ikiwemo mradi uliofadhiliwa na Benki ya Exim ya India;

ii. Kuongeza hifadhi ya maji kupitia ujenzi wa matangi ya kisasa ya ZincAlumn ya ujenzi wa muda mfupi zaidi ikilinganishwa na matangi ya maji ya zege kwa Unguja na Pemba pamoja na uchimbaji, uboreshaji na ukarabati wa visima vya maji kwa Unguja na Pemba;

iii. Kuongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa maji Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na utekelezaji wa mradi wa Ukarabati na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji kupitia Kampuni ya NEC;

iv. Kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji Mkoa wa Kusini Unguja katika skimu tano (5) zikiwemo Kizimkazi, Bwejuu, Jambiani, Pagali na Cheju;

v. Kuanza utekelezaji wa Skimu tisa (9) za Pemba ambazo ni Pandani, Ole, Muambe-Kengeja, Madenjani, Wingwi, Chokocho, Sizini, Chambani Wawi pamoja na uendelezaji wa miundombu ya maji katika skimu saba

(7) za Pemba ambazo ni Ngwachani, Mtambwe, Junguni, Mzambarauni, Ziwani, Mjimbini, na Gombani kupitia Kampuni ya Jenkins Asia Ltd;

vi. Kupunguza upotevu wa maji kwa kubadilisha mabomba chakavu na kuziba mivujo na kuendelea kusimamia ulipaji wa fidia na maandalizi ya maeneo kwa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maji inayoanza utelekezaji wake kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027;

vii. Kuimarisha uzalishaji wa umeme kwa kuongeza na kuboresha vyanzo vya uhakika (baseload), pamoja na kupanua na kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji ili kupunguza upotevu na kuongeza ufanisi wa huduma; na

viii. Kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu na teknolojia za kisasa za uhifadhi na usimamizi wa umeme, pamoja na kuboresha upatikanaji wa umeme Unguja na Pemba, ikijumuisha uimarishaji wa miundombinu ya nyaya za baharini.

153. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itatekeleza vipaumbele hivyo kupitia Fungu 015 lenye Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) zifuatazo: -

***Programu Kuu P0301: Usimamizi wa Huduma za Maji***

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo moja (1)

ambayo ni Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji.

154. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za usambazaji wa maji safi na usimamizi wa usafi wa mazingira (maji taka) kwa wote;
ii. Kuhifadhi na kusimamia rasilimali maji Unguja na Pemba;
iii. Kuanzisha na kusimamia mfumo wa taarifa za ubora na wingi wa rasilimali maji Unguja na Pemba;
iv. Kuandaa miongozo ya uendelezaji wa rasilimali maji na usafi wa mazingira;
v. Kuandaa tafiti mbali mbali za vyanzo vya maji katika sekta ya maji safi na maji taka;

vi. Kuandaa mfumo wa utoaji vibali na leseni ya uendelezaji rasilimali maji na maji taka; na

vii Kuanzisha jumuia shirikishi za uhifadhi maji katika shehia na kuwajengea uwezo juu ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali maji.

155. **Mheshimiwa Spika,** programu hii itaenda sambamba na utekelezaji unaofanywa na Kampuni ya "Rand Water Zanzibar" inayotekeleza shughuli za ZAWA. Kampuni hiyo itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i Kusimamia, kuimarisha na kuiendesha miundombinu ya Maji kwa kuwaunganishia wananchi;

ii Kufanya uwekezaji wa teknolojia na miundombinu ya kusambazia maji;

iii Kukusanya mapato kutokana na utoaji huduma ya maji Kuwajengea uwezo watendaji pamoja na Kuzijengea uwezo Ofisi za Wilaya; na

iv Kuwekeza katika miradi mipya ya maji na kuimarisha miundombinu iliyopo.

156. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji iweze kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza Lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 179.9 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 2.10 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 3.62 milioni** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 9.21 bilioni** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na **TZS. 168.23 bilioni** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo.

***Programu Kuu P0302: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini***

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili ambazo ni: -

i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati; na

ii. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini.

157. **Mheshimiwa Spika,** programu hii itatekelezwa kupitia Idara ya Nishati na Madini na ikihusisha utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO). Kupitia Idara ya Nishati na Madini Programu hii itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa elimu ya matumizi ya Nishati Mbadala, Nishati Sanifu na Nishati za Kisasa kwa jamii hususan wanawake;
ii. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka 2025;
iii. Kufanya tafiti za vyanzo tofauti vya nishati;
iv. Kusimamia Ufuatiliaji wa Miradi ya Nishati; na
v. Utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya upatikanaji wa Maliasili Zisizorejesheka.

158. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupitia Programu hii itatekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kupeleka umeme Vijijini na Mashambani;
ii. Kuongeza idadi ya wateja wapya;
iii. Kuondosha tatizo la umeme mdogo kwa maeneo ambayo yamezidiwa; na
iv. Kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuwafungia wateja pre-paid smart meter.

159. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linatarajia kukusanya jumla ya **TZS. 344.24 bilioni** kupitia vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni; mauzo ya umeme, mapato ya huduma nyenginezo, mchango wa Serikali na makusanyo ya madeni ya wateja. Shirika limekadiria kutumia jumla ya **TZS. 265.26 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Aidha, ifikapo tarehe 30 Juni, 2027 Shirika linatarajia kupata bakaa ya jumla ya **TZS. 64.44 bilioni.**

160. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha Nyenzo za Udhibiti wa huduma za Maji na Nishati;
ii. Kuimarisha upatikanaji, endelevu na salama wa huduma za maji na nishati;
iii. Kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi;
iv. Kuimarisha uwezo wa Taasisi wa kudhibiti Huduma za Maji na Nishati; na
v. Kutoa elimu pamoja na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

161. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027 ZURA imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 50.12 bilioni** kutokana na tozo la Mamlaka "Regulatory Levy" inayotokana na mafuta, gesi ya kupikia (LPG) mapato ya leseni na mapato mengineyo. Aidha, imekadiria kutumia jumla ya **TZS. 50.12 bilioni** kwa ajili ya kazi za kawaida, kazi za Maendeleo, Ulipaji wa deni na Mchango wa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **TZS. 9.81 bilioni** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS. 5.19 bilion**i kwa kazi za Maendeleo, **TZS. 6.09 bilioni** kwa ajili ya Mishahara, **TZS. 24.03 bilioni** kwa ajili ya ulipaji wa deni la PBZ na **TZS. 5.00 bilioni** kwa ajili ya Mchango wa Mamlaka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

162. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini iweze kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza Lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 291.37 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara na kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 332.63 milioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 458.00 milio**ni kwa ajili ya mishahara na **TZS. 290.58 bilioni** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo.

**Programu Kuu P0303: Uratibu wa Mipango, Uendeshaji na Utawala wa WMNM**

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo tatu ambazo ni: -

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa WMNM;
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa WMNM;
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za WMNM-Afisi Kuu Pemba.

163. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa huduma za uendeshaji wa Ofisi katika Wizara ya Maji Nishati na Madini;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na ya ndani;
iii. Kuandaa, Kusimamia na Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo yake;
iv. Kufuatilia na Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera za Wizara ya Maji, Nishati na Madini;
v. Kukusanya na kuchambua takwimu za utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Maji, Nishati na Madini; na
vi. Kuratibu na kukuza mashirikiano ya kisekta na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara.

164. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara iweze kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 4.10 bilioni** kwa matumizi ya kazi za kawada na mishahara. Kati ya fedha hizo, **TZS. 1.95 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS. 2.15 bilioni** kwa ajili ya mishahara.

165. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutekeleza Programu zake na kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Wizara kwa Fungu 015 lenye jumla ya **TZS. 475.39 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 4.38 bilioni** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 2.97 bilioni** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 9.21 bilioni** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, **TZS. 458.81 bilioni** (SMZ **TZS. 315.42** na Wahisani **TZS. 143.39**) kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa kila Programu umeainishwa katika ***Kimbatisho Namba 10.***

166. **Mheshimiwa Spika**, naomba idhini ya kukusanya TZS. 25.72 bilioni kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato yatokanayo na Maliasili Zisizorejesheka.

## E. HITIMISHO

167. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyotekeleza kwa ufanisi Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020- 2050 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025-2030) kwa vitendo.

168. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza kwa dhati wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya Hotuba hii akiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Seif Kombo Pandu, Katibu Mkuu Ndugu Joseph John Kilangi, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwanajuma Majid Abdullah, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Idara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu.


169. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kutupatia, uzalendo na uchapakazi wao umesaidia kuweza kuzitatua kwa pamoja changamoto za ukosefu wa maji, umeme na madini zinazowakabili wananchi wa Zanzibar.

170. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kushukuru na kuthamini michango na ushirikiano kutoka kwa washirika na wadau wetu wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi wakiwemo Waheshimiwa Mabalozi wa Nchi mbali mbali, Taasisi ya Usimamizi na Ufuatiliaji wa Utendaji Serikalini (ZPDB), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Benki ya CRDB, Benki ya NMB, Benki ya Exim ya India, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya ABSA, Benki ya Uwekezaji wa Miundombinu ya Asia (AIIB), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Fedha Duniani (IMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya JICA (Japan), GWPSA na GWPTZ, GiZ (Ujerumani), NEC (Oman), NORAD (Norway), SIDA (Sweden), UNDP, UNICEF, Action Aid, Uongozi Institute na washirika wengine wa maendeleo.

171. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa kuwasilisha Hotuba hii.

172. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukrani hizo, sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, kutushauri na hatimae waipitishe Bajeti hii ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ili tuweze kutekeleza majukumu ya kuwapatia huduma bora za maji, nishati na Madini wananchi wetu.

173. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.



........................................................

**(Mheshimiwa Nadir Abdullatif - Alwardy)**
**Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar**
**Zanzibar**

# VIAMBATISHO

## *Kiambatisho Namba 1: Muhtasari wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | MATUMIZI | BAJETI ILIYOPANGWA KWA MWAKA WA FEDHA, 2025/2026 | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI, 2025/2026 | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Usimamizi wa Huduma za Maji | Kusimamia Huduma na Upatikanaji wa Maji Safi na Salama | Idara ya Maendeleo ya Maji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 543,010,000.00 | | 543,010,000.00 | 144,449,712.00 | | 144,449,712.00 | 26.60 |
| | | | Fedha za Mishahara | 307,435,000.00 | . | 307,435,000.00 | 211,109,350.00 | | 211,109,350.00 | 68.67 |
| | | | Ruzuku ya Mshahara | 10,110,400,000.00 | | 10,110,400,000.00 | 6,721,190,812.00 | | 6,721,190,812.00 | 66.48 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **10,960,845,000.00** | **-** | **10,960,845,000.00** | **7,076,749,874.00** | **-** | **7,076,749,874.00** | **64.56** |
| | Kuimarisha huduma za Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Mamla ka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Fedha za Miradi ya Maendeleo | 25,034,560,000.00 | 129,523,229,000.00 | 154,557,789,000.00 | 7,402,233,220.00 | | 7,402,233,220.00 | 4.79 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **35,995,405,000.00** | **129,523,229,000.00** | **165,518,634,000.00** | **14,478,983,094.00** | **-** | **14,478,983,094.00** | **8.75** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 1** | | | **35,995,405,000.00** | **129,523,229,000.00** | **165,518,634,000.00** | **14,478,983,094.00** | **-** | **14,478,983,094.00** | **8.75** |
| Usimamizi wa huduma za Nishati na Madini | Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | Idara ya Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 316,941,000.00 | | 316,941,000.00 | 49,506,000.00 | | 49,506,000.00 | 15.62 |
| | | | Fedha za Mishahara | 889,116,000.00 | | 889,116,000.00 | 231,296,486.00 | | 231,296,486.00 | 26.01 |
| | | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | Fedha za Miradi ya Maendeleo | 40,355,685,000.00 | 10,443,290,000.00 | 50,798,975,000.00 | 68,319,711,797.00 | 1,798,625,087.39 | 70,118,336,884.39 | 138.03 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **41,561,742,000.00** | **10,443,290,000.00** | **52,005,032,000.00** | **68,600,514,283.00** | **1,798,625,087.39** | **70,399,139,370.39** | **135.37** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 2** | | | **41,561,742,000.00** | **10,443,290,000.00** | **52,005,032,000.00** | **68,600,514,283.00** | **1,798,625,087.39** | **70,399,139,370.39** | **135.37** |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uendes haji na Uratibu wa Mipang o ya WMNM | Utawala na Uendes haji wa WMNM | Utumis hi na Uendes haji | Fedha za Matum izi Mengin eyo | 569,232,000.00 | | 569,232,000.00 | 170,928,393.00 | | 170,928,393.00 | 30.03 |
| | | | Fedha za Mishah ara | 792,434,000.00 | | 792,434,000.00 | 1,104,906,305.00 | | 1,104,906,305.00 | 139.43 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **1,361,666,000.00** | **-** | **1,361,666,000.00** | **1,275,834,698.00** | **-** | **1,275,834,698.00** | **93.70** |
| | Uratibu wa Mipang o, Sera na Utafiti | Idara ya Mipang o, Sera na Utafiti | Fedha za Matum izi Mengin eyo | 403,655,000.00 | 200,000,000.00 | 603,655,000.00 | 127,656,500.00 | 194,069,680.00 | 321,726,180.00 | 53.30 |
| | | | Fedha za Mishah ara | 156,207,000.00 | | 156,207,000.00 | 182,317,450.00 | | 182,317,450.00 | 116.72 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **559,862,000.00** | **200,000,000.00** | **759,862,000.00** | **309,973,950.00** | **194,069,680.00** | **504,043,630.00** | **66.33** |
| | Uratbu wa Utekele zaji wa Shughul i za WMNM - Pemba | Afisi Kuu - Pemba | Fedha za Matum izi Mengin eyo | 405,162,000.00 | | 405,162,000.00 | 111,408,650.00 | | 111,408,650.00 | 27.50 |
| | | | Fedha za Mishah ara | 775,408,000.00 | | 775,408,000.00 | 389,299,862.50 | | 389,299,862.50 | 50.21 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **1,180,570,000.00** | **-** | **1,180,570,000.00** | **500,708,512.50** | **-** | **500,708,512.50** | **42.41** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 3** | | | **3,102,098,000.00** | **200,000,000.00** | **3,302,098,000.00** | **2,086,517,160.50** | **194,069,680.00** | **2,280,586,840.50** | **69.06** |
| | **JUMLA YA FUNGU NO3** | | | **80,659,245,000.00** | **140,166,519,000.00** | **220,825,764,000.00** | **85,166,014,537.50** | **1,992,694,767.39** | **87,158,709,304.89** | **39.47** |

### *Kiambatisho Namba 2:Mapato yatokanayo na Maliasili Zisizorejesheka*

| | | Q1 | | Q2 | | Q3 | | JULAI - MACHI 2025/2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KASMA** | **CHANZO CHA MAPATO MWAKA WA FEDHA 2024/2025** | **MAKADIRIO** | **MAPATO HALISI** | **MAKADIRIO** | **MAPATO HALISI** | **MAKADIRIO** | **MAPATO HALISI** | **MAKADIRIO** | **MAPATO HALISI** | **%** |
| **OFISI KUU PEMBA** | | | | | | | | | | |
| 1422010 | VIBALI | 16,500,000.00 | 13,412,408.00 | 16,500,000.00 | 23,457,808.00 | 16,500,000.00 | 20,441,000.00 | 49,500,000.00 | 57,311,216.00 | 115.78% |
| 1430001 | FAINI | 3,000,000.00 | 3,025,000.00 | 3,000,000.00 | - | 3,000,000.00 | 3,900,000.00 | 9,000,000.00 | 6,925,000.00 | 76.94% |
| 1422118 | USAJILI NA LESENI | 18,000,000.00 | 4,500,000.00 | 18,000,000.00 | 3,743,000.00 | 18,000,000.00 | 12,940,000.00 | 54,000,000.00 | 21,183,000.00 | 39.23% |
| 1422023 | ADA YA MAWE NA KOKOTO | 292,968,750.00 | 132,916,000.00 | 292,968,750.00 | 407,133,500.03 | 292,968,750.00 | 311,402,000.00 | 878,906,250.00 | 851,451,500.03 | 96.88% |
| 1422023 | ADA YA MCHANGA | 343,919,750.00 | 153,314,000.00 | 343,919,750.00 | 366,373,000.00 | 343,919,750.00 | 276,752,000.00 | 1,031,759,250.00 | 796,439,000.00 | 77.19% |
| | **JUMLA** | **674,388,500.00** | **307,167,408.00** | **674,388,500.00** | **800,707,308.03** | **674,388,500.00** | **625,435,000.00** | **2,023,165,500.00** | **1,733,309,716.03** | **85.67%** |
| **IDARA YA NISHATI NA MADINI** | | | | | | | | | | |
| 1422010 | VIBALI | 41,500,000.00 | 80,187,500.00 | 41,000,000.00 | 64,279,000.00 | 41,000,000.00 | 119,799,400.00 | 123,500,000.00 | 264,265,900.00 | 213.98% |
| 1430001 | FAINI | 48,000,000.00 | 51,886,000.00 | 49,000,000.00 | 141,075,000.00 | 58,000,000.00 | 83,881,000.00 | 155,000,000.00 | 276,842,000.00 | 178.61% |
| 1422118 | USAJILI NA LESENI | 67,500,000.00 | 21,307,334.00 | 67,500,000.00 | 8,688,000.00 | 67,500,000.00 | 105,633,000.00 | 202,500,000.00 | 135,628,334.00 | 66.98% |
| 1422023 | ADA YA MAWE NA KOKOTO | 1,483,372,000.00 | 1,758,368,322.00 | 1,454,523,000.00 | 1,641,736,376.00 | 1,349,374,000.00 | 1,803,801,834.00 | 4,287,269,000.00 | 5,203,906,532.00 | 121.38% |
| 1422023 | ADA YA MCHANGA | 2,956,745,000.00 | 2,921,926,700.00 | 2,899,047,000.00 | 2,184,172,966.72 | 2,913,748,000.00 | 2,571,090,486.00 | 8,769,540,000.00 | 7,677,190,152.72 | 87.54% |
| NEW | *MAJI | - | - | - | 2,380,000.00 | - | 3,780,000.00 | - | 6,160,000.00 | #DIV/0! |
| | **JUMLA** | **4,597,117,000.00** | **4,833,675,856.00** | **4,511,070,000.00** | **4,042,331,342.72** | **4,429,622,000.00** | **4,687,985,720.00** | **13,537,809,000.00** | **13,563,992,918.72** | **100.19%** |
| | **JUMLA KUU** | **5,271,505,500.00** | **5,140,843,264.00** | **5,185,458,500.00** | **4,843,038,650.75** | **5,104,010,500.00** | **5,313,420,720.00** | **15,560,974,500.00** | **15,297,302,634.75** | **98.31%** |

***Kiambatisho Namba 3: Vijiji vilivyopatiwa huduma ya umeme***

| Nam. | UNGUJA | Nam. | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1. | Chaani Ketwa | 1. | Mzambarau Mboko |
| 2. | Kizimkazi | 2. | Marekeni Vitongoji |
| 3. | Jambiani | 3. | Shemka Ngomani |
| 4. | Cheju | 4. | Mjini Wingi |
| 5. | Muyuni | 5. | Kwa Mgogo Sipwesi, |
| 6. | Uzi Shamba | 6. | Momoni |
| 7. | Pete | 7. | Rasini Gando |
| 8. | Muyuni A | 8. | Kinyasini Mtambwe (Mayatima) |
| 9. | Jendele Maguruweni | | |
| 10. | Vijiji vya Kidoti | | |
| 11. | Muyuni | | |
| 12. | Bwejuu Mashambani | | |
| 13. | Kijibwe Mtu | | |
| 14. | Muyuni Mashambani | | |
| 15. | Mtule Mashamabani | | |

***Chanzo: ZECO, 2026***

***Kiambatisho Namba 4: Maeneo yaliyokuwa na tatizo la umeme mdogo ambayo yameshapelekewa ya huduma za umeme***

| **Nam.** | **Unguja** | **Nam.** | **Pemba** |
|---|---|---|---|
| 1 | Mwera Gudini | 1 | Tange Kangani |
| 2 | Kitope M/Majogoo | 2 | Mjini Wingwi |
| 3 | Zuri | 3 | Kiuyu Mbuyuni |
| 4 | Potoa | 4 | Masota kwa Kachumbiru |
| 5 | Bwejuu Tangini | 5 | Bopwe Wete |
| 6 | Jumbi Mji Mpya | 6 | Madungu Cossovo |
| 7 | Bwejuu kwa Hamza | 7 | Istikama Mkoani |
| 8 | Mbweni kwa Jastuma | 8 | Connecting |
| 9 | Bumbwini Misufini | | |
| 10 | Kisaka saka | | |
| 11 | Kisauni Jamboma | | |
| 12 | Mwera Mkahawa wa Wajane | | |
| 13 | Michikichini | | |
| 14 | Bwejuu kwa Hamza | | |
| 15 | Chunga | | |
| 16 | Potoa | | |
| 17 | Binguni 01 | | |
| 18 | Binguni 01 | | |
| 19 | Mtule | | |
| 20 | Mfenesini Madukani | | |
| 21 | Maji Mekundu | | |
| 22 | Jumbi Kibondeni | | |
| 23 | Magogoni Mikarafuuni | | |
| 24 | Mkanyageni | | |

***Chanzo: ZECO, 2026***

***Kiambatisho Namba 5: Hali ya uingizwaji na matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa (Julai - Machi) 2025/2026***

| HALI YA UINGIZWAJI NA MATUMIZI YA MAFUTA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2025 - MACHI 2026) (LITA) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWEZI** | | **PETROLI** | **DIZELI** | **MAFUTA YA TAA** | **JET A-1** | **JUMLA** |
| JULAI 2025 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 8,677,319 | 7,589,719 | 180,136 | 8,558,246 | 25,005,420 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,130,176 | 6,261,585 | 122,500 | 7,370,273 | 22,884,534 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **294,522** | **201,987** | **3,952** | **237,751** | **738,211** |
| AGOSTI 2025 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 15,527,747 | 9,049,194 | 129,980 | 5,319,781 | 30,026,702 |
| | Matumizi kwa mwezi | 11,695,852 | 8,672,821 | 85,300 | 6,396,500 | 26,850,473 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **377,286** | **279,768** | **2,752** | **206,339** | **866,144** |
| SEPTEMBA 2025 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 11,453,773 | 9,573,080 | 126,545 | 6,894,367 | 28,047,765 |
| | Matumizi kwa mwezi | 11,668,479 | 8,579,205 | 106,500 | 6,055,500 | 26,409,684 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **388,949** | **285,974** | **3,550** | **201,850** | **880,323** |
| OKTOBA 2025 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 9,235,306 | 7,698,393 | | 9,527,311 | 26,461,010 |
| | Matumizi kwa mwezi | 11,478,483 | 8,392,927 | 87,500 | 8,005,704 | 27,964,614 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **382,616** | **279,764** | **2,917** | **266,857** | **932,154** |
| NOVEMBA 2025 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 12,812,264 | 9,164,093 | | 2,661,891 | 24,638,248 |
| | Matumizi kwa mwezi | 10,768,224 | 8,823,077 | 119,500 | 4,605,000 | 24,315,801 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **358,941** | **294,103** | **3,983** | **153,500** | **810,527** |
| DISEMBA 2025 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 12,258,974 | 6,619,284 | 129,160 | 7,204,024 | 26,211,442 |
| | Matumizi kwa mwezi | 12,947,065 | 9,954,886 | 91,000 | 6,167,852 | 29,160,803 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **431,569** | **331,830** | **3,033** | **205,595** | **972,027** |
| JANUARI 2026 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 10,096,172 | 9,617,424 | 306,000 | 4,283,645 | 24,303,241 |
| | Matumizi kwa mwezi | 12,329,462 | 10,747,312 | 105,500 | 5,983,000 | 29,165,274 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **397,725** | **346,687** | **3,403** | **193,000** | **940,815** |
| FEBRUARI 2026 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 12,897,833 | 9,234,534 | - | 5,181,653 | 27,314,020 |
| | Matumizi kwa mwezi | 11,510,997 | 9,464,346 | 78,200 | 5,881,000 | 26,934,543 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **371,322** | **305,301** | **2,523** | **189,710** | **868,856** |
| MACHI 2026 | Yaliyoingizwa kwa mwezi | 15,591,340 | 11,624,522 | 2,526,525 | 1,012,913 | 30,755,300 |
| | Matumizi kwa mwezi | 10,688,757 | 9,581,255 | 128,900 | 4,934,497 | 25,333,409 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 344,799 | 309,073 | 4,158 | 159,177 | 817,207 |
| **JUMLA YA MAFUTA YALIOINGIZWA KWA KILA BIDHAA** | | **108,550,728** | **80,170,243** | **3,398,346** | **50,643,831** | **242,763,148** |
| **JUMLA YA MAFUTA YALIOUZWA KWA KILA BIDHAA** | | **102,217,495** | **80,477,414** | **924,900** | **55,399,326** | **239,019,135** |

***Chanzo: ZURA, 2026***

***Kiambatisho Namba 6: Vituo vya mafuta kwa kipindi cha Julai - Machi, 2026***

| | WILAYA | VIKONGWE | VIPYA | GAPCO | UP | ZP | GBP | PUMA | BINAFSI | JUMLA | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UNGUJA** | **MJINI** | 12 | 0 | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 3 | 12 | **127** |
| | **MAGHARIBI "A"** | 17 | 2 | 3 | 3 | 2 | 0 | 0 | 11 | 19 | |
| | **MAGHARIBI "B"** | 21 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 1 | 15 | 21 | |
| | **KATI** | 14 | 0 | 1 | 3 | 2 | 0 | 0 | 8 | 14 | |
| | **KUSINI** | 11 | 1 | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 6 | 12 | |
| | **KASKAZINI "A"** | 17 | 0 | 2 | 1 | 5 | 0 | 0 | 9 | 17 | |
| | **KASKAZINI "B"** | 9 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 6 | 9 | |
| | **JUMLA NDOGO** | | | **14** | **14** | **15** | **2** | **1** | **58** | **104** | |
| **PEMBA** | **MICHEWENI** | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 5 | |
| | **WETE** | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 6 | |
| | **CHAKECHAKE** | 8 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 8 | |
| | **MKOANI** | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 4 | |
| | **JUMLA NDOGO** | **21** | **2** | **1** | **0** | **0** | **0** | **0** | **22** | **23** | |

***Chanzo: ZURA, 2026***

***Kiambatisho Namba 7: Mwenendo wa bei za Mafuta zilizotangazwa na Mamlaka kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025/2026***

| MWEZI | PETROLI (TZS) | DIZELI (TZS) | MAFUTA YA TAA (TZS) | JET- A 1(TZS) |
|---|---|---|---|---|
| JULAI 2025 | 2,996 | 2,907 | 3,000 | 2,370 |
| AGOSTI 2025 | 2,978 | 3,076 | 3,000 | 2,421 |
| SEPTEMBA 2025 | 2,943 | 2,993 | 3,000 | 2,502 |
| OKTOBA 2025 | 2,809 | 2,944 | 3,000 | 2,343 |
| NOVEMBA 2025 | 2,868 | 3,004 | 3,000 | 2,405 |
| DISEMBA 2025 | 2,815 | 2,944 | 3,000 | 2,376 |
| JANUARI 2026 | 2,813 | 2,858 | 2,900 | 2,485 |
| FEBUARI 2026 | 2,985 | 2,962 | 2,900 | 2,537 |
| MACHI 2026 | 2,942 | 2,952 | 2,900 | 2,368 |

***Chanzo: ZURA, 2026***

*Kiambatisho Namba 8: Gesi iliyoingizwa na kutumika kwa kipindi cha Julai -Machi, 2026*

| UINGIZWAJI NA MATUMIZI YA GESI YA KUPIKIA (LPG), KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA KUANZIA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWEZI/KAMPUNI** | | **JULAI** | **AGOSTI** | **SEPTEMBA** | **OKTOBA** | **NOVEMBA** | **DISEMBA** | **JANUARI** | **FEBRUARI** | **MACHI** | **JUMLA** |
| LAKE GAS (Kg) | UINGIZWAJI | 78,820 | 106,380 | 87,660 | 67,325 | 82,140 | 85,546 | 80,000 | 0 | 0 | 587,871 |
| | MATUMIZI | 85,398 | 83,220 | 90,875 | 67,600 | 86,380 | 79,430 | 83,200 | 82,027 | 60,765 | 718,895 |
| ORYX GAS TANZANIA LIMITED (Kg) | UINGIZWAJI | 697,871 | 1,000,105 | 1,000,084 | 1,000,220 | 0 | 2,000,779 | 586,783 | 1,040,991 | 995,897 | 8,322,730 |
| | MATUMIZI | 971,044 | 1,000,475 | 895,652 | 928,000 | 982,000 | 1,035,000 | 1,018,312 | 1,081,786 | 981,334 | 8,893,603 |
| TAIFA GAS ZANZIBAR LTD(Kg) | UINGIZWAJI | 137,090 | 163,770 | 160,506 | 166,460 | 146,450 | 214,440 | 181,820 | 130,119 | 154,116 | 1,454,771 |
| | MATUMIZI | 146,029 | 154,450 | 156,409 | 155,447 | 143,942 | 148,661 | 157,604 | 160,251 | 175,083 | 1,397,876 |
| ALNABAHAN GAS SUPPLY - O-GAS (Kg) | UINGIZWAJI | 16,500 | 17,300 | 17,600 | 18,000 | 29,040 | 33,337 | 28,357 | 24,300 | 13,500 | 197,934 |
| | MATUMIZI | 16,400 | 17,800 | 18,000 | 20,000 | 29,442 | 31,069 | 29,157 | 25,360 | 16,340 | 203,568 |
| **JUMLA** | **UINGIZWAJI** | **930,281** | **1,287,555** | **1,265,850** | **1,252,005** | **257,630** | **2,334,102** | **876,960** | **1,195,410** | **1,163,513** | **10,563,306** |
| | **MATUMIZI** | **1,218,871** | **1,255,945** | **1,160,936** | **1,171,047** | **1,241,764** | **1,294,160** | **1,288,273** | **1,349,424** | **1,233,522** | **11,213,942** |

***Chanzo: ZURA, 2026***

***Kiambatisho Namba 9: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini***

## 1.Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji Huduma za Usambazaji Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar ili kufanikisha malengo yalioainishwa katika mikakati mbalimbali ya Serikali. Utekelezaji wa shughuli za mradi huu utahusisha Serikali pamoja na Washirika wa Maendeleo. Mradi huu unagharimu jumla ya Dola za kimarekani milioni 35. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya **TZS 16.16 bilioni** (**TZS 2.5 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 13.65 bilioni** kutoka Benki ya EXIM-India). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 mradi upo katika hatua za awali za utekelezaji kwa ajili ya kumpata mshauri elekezi na mkandarasi.

## 2.Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Zanzibar

Programu hii imelenga kuondoa changamoto zinazohusiana na sekta ya maji kwa kutekeleza miradi kupitia usimamizi wa wizara. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni mradi wa maji Kengeja na Mradi wa Ujenzi wa Matangi ya zink Aluminium katika maeneo ya Kengeja, Raha, Mtambwe Kaskazini na Kusini. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya **TZS 15.77 bilioni** kutoka Serikalini.

## 3.Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi

## (ZUWDIFP)

Mradi huu una lengo la kuongeza uzalishaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma hiyo. Mradi utatekelezwa katika maeneo ya Welezo juu, Welezo Magharibi na Migombani. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya **TZS 41.49 bilioni** (**TZS 1.5 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 39.94 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo JICA). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 fedha zilizotumika ni kwa ajili ya malipo ya utayarishaji wa tathmini ya athari za mazingira jumla ya **TZS 59.6 milioni**

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya tekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa taarifa ya kina ya kitaalamu (Details design) ya mradi. | Asilimia ya taarifa iliyoandaliwa. | 100 | 100 | 100 | Kazi hiyo imekamilika. |
| Kuandaa mpango na utaratibu wa manunuzi kwa ajli ya kupata Mkandarasi. | Asilimia ya mpango na utaratibu wa manunuzi ulioandaliwa. | 100 | 70 | 70 | Mpango wa manunuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi unaendelea. |
| Kufanya tathmini kwa ajili ya kumtafuta Mkandarasi | Asilimia ya tathmini iliyofanyika. | 100 | 0 | 0 | Kazi ya tathmini kwa ajili ya kumtafutaMkandarasi inatarajiwa kuanza ndani ya muda mfupi baada ya kukamilika taratibu za zabuni |
| Kuandaa Mikataba kwa ajili ya Mkandarasi. | Asilimia ya mikataba iliyoandaliwa. | 100 | 65 | 65 | Mshau elekezi Ameshaandaa tender document kwa ajili ya Mkandarasi, ambayo kwa sasa ipo kwa washirika wa maenmdeleo JICA kwa ajili ya kuweka mapendekezo.<br>Ripoti ya EIA imeandaliwa, ili kuweza kukamilisha taratibu na masharti ya mradi. |

49

### 4. Mradi wa Usalama wa Maji na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mjini (GIZ)

Mradi huu una lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamiaji wa usalama na upatikanaji wa maji nchini. Mradi huu umelenga kutekeleza maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kusaidia Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika usimamizi wa mikakati na miongozo ya mageuzi, kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa kimazingira na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar ili iweze kujiendesha kibiashara. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya **TZS 2.00 bilioni** kutoka Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 fedha zote zimetumika.

### 5 .Programu ya UNICEF

Programu hii inatekelezwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Maji Zanzibar na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF). Lengo kuu la programu hii ni kutambua idadi ya visima binafsi pamoja na kutoa vifaa na dawa za kutibu maji. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia **TZS 40,000,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 Fedha zote zimepatikana na kutumika kwa kununulia dawa za kutibia maji, hatua inayosaidia upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

### 6.Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Huduma ya Maji Safi na Salama Mkoa wa Kaskazini Unguja kupitia Kampuni ya (NEC)

Mradi unatekelezwa katika Mkoa wa kaskazini Unguja kwa skimu ya Mahonda, Nungwi na Kiwengwa. Vile vile, sehemu ya Mkoa wa Kusini Unguja katika skimu ya Machui.Mradi unagharimu jumla ya **26,309,041.20 USD**. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi wa National Energy Center (NEC) – kutoka OMAN kupitia utaratibu wa EPC+F. Uchimbaji wa visima vitatu (3) umekamilika (Mahonda viwili na Kilindi kimoja), visima 51 vimekarabatiwa na kazi nyengine zinaendelea ikiwemo kuwaunganishia huduma ya maji wananchi, ulazaji mabaomba, ufungaji wa solar panel katika visima na ununuzi wa vifaa ikiwemo mita za maji.

## 7.Mradi wa Upembuzi Yakinifu Juu ya Usalama Wa Maji

Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW). Mradi umepangiwa kutumia EURO Milioni 25 kwa kazi za Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kisiwani Pemba. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 mradi huu umepangiwa jumla ya **TZS 71.4 bilioni (TZS 2.6 bilioni** kutoka Serikalini na **TZS 68.8 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 hakuna fedha zilizotumika. Hata hivyo, taratibu za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya utayarishaji wa michoro, ramani, usanifu, uchambuzi wa gharama za ujenzi pamoja na uandaaji wa nyaraka za zanubi y akumpata Mkandarasi zinaendelea.

## 8.Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali Maji Chini ya Ardhi

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kupitia msaada wa kiufundi kutoka JICA. Lengo la mradi ni kuongeza taaluma za kiufundi kwa watendaji na taasisi katika usimamizi wa maji chini ya ardhi na usambazaji maji. Mradi umefanikiwa kuandaaa Ripoti ya Tathmini ya maji chini ya Ardhi kwa Skimu ya Kisauni-Kwarara na Maungani zimetayarishwa. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 mradi umepangiwa jumla ya **TZS 1.6 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 jumla ya **TZS 1.20 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **75**.

## 9.Mradi wa Usalama wa Maji na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mjini (GIZ)

Mradi huu una lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamiaji wa usalama na upatikanaji wa maji nchini. Mradi unatekelezwa katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni; kusaidia Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika usimamizi wa mikakati na miongozo ya mageuzi; kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa kimazingira; na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar ili iweze kujiendesha kibiashara. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya **TZS 2.00 bilioni** kutoka GIZ. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 fedha zote zimetumika.

Mradi umekamilisha Mapitio ya Sheria ya Maji Nam. 3 ya 2006, Aidha; utayarishaji wa Miongozo ya utoaji wa vibali vya maji taka, uandaaji wa mwongozo uchimbaji maji ya chini ya ardhi, upangaji wa mji kwa pamoja (Joint Town Plan) katika Mji wa Chake Chake, Ubunifu wa mradi wa usambazaji na usakinishaji wa mifumo ya nishati ya jua kwa vituo vya kusukuma maji, Utafiti wa uvunajai wa maji ya mvua (RWH).

**10 .Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme**

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme kwa usambazaji wa laini, ununuzi wa transfoma, mita, nguzo katika maeneo ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya **TZS 7 bilioni** kutoka Serikalini ambapo Vijiji 61 vilisambazwa umeme (33 Unguja na 28 Pemba). Kazi ya usambazaji umeme inaendelea katika maeneo mengine. Jumla ya nguzo za Umeme1676 zimebadilishwa (Pemba ni 521 na Unguja ni 1,155). Aidha, Jumla ya wateja wapya 38,400 wameunganishwa (Pemba 15,200 na Unguja 23,200).

**11.Mradi wa Kuandaa Mpango Mkuu wa Maji Safi, Maji Machafu na Rasilimali Maji**

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW). Mradi umepangiwa kutumia EURO Milioni 1.4 kwa kazi za kuandaa Mipango Mikuu mitatu ya Maji safi, maji machafu na rasilimali maji. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 mradi huu umepangiwa jumla ya **TZS 3.36 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 hakuna fedha zilizotumika kwa mradi huu. Hata hivyo Mshauri Elekezi amepatikana na ameanza kazi za matayarisho ya utekelezaji.

**12.Mradi wa Ulazaji wa Nyaya za Chini ya Bahari (AfDB)**

Mradi huu umeandaliwa kwa ajili ya kuondoa tatizo la miundombinu iliyozidiwa ya kupokelea umeme kutoka Tanzania Bara na kusawazisha kuwa katika kiwango kinachohitajika. Mradi unalenga kulaza nyaya mpya za chini ya bahari (Submarine cable) Unguja kwa kiwango cha 270MW/220kVA na Pemba 100MW/132kVA pamoja na kuwaunganishia wananchi umeme kwa kiwango kidogo cha malipo (last miles connection) na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia. Mradi unatarajiwa kutekelezwa takribani miezi 33 kupitia

Awamu tatu: Kabla ya ujenzi – miezi 8, Wakati wa ujenzi – miezi 23, Baada ya ujenzi – miezi 2). Mradi unatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia ufadhili wa Mkopo nafuu kutoka AfDB kwa thamani ya jumla ya takribani **USD 282.57 milioni**. Mradi upo katika hatua za awali za utekelezaji. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya **TZS 3.96 bilioni** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 hakuna fedha zilizotumika kwa mradi huu.

**13. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)**

Mradi huu ni mkopo kutoka Benki ya Dunia wenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani milioni 142 kwa lengo la kuimarisha sekta ya nishati na upatikanaji wa huduma ya umeme Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ambao unahusisha ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua kwa kiwango cha Megawati 18 (18 MW) katika eneo la Makunduchi, kuimarisha miundombinu ya usafirishaji umeme ikiwemo ujenzi wa njia kuu ya usafirishaji umeme ya msongo wa 132kV yenye ukubwa wa masafa ya kilomita mia moja (100km) itakayoanzia kutoka kituo kikuu cha umeme Mtoni hadi Kaskazini na Kusini mwa kisiwa cha Unguja, kuongeza upatikananji wa huduma ya umeme kwa wananchi wa Zanzibar na kuwajengea uwezo watendaji katika Sekta ya Nishati.

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| **USHAURI ELEKEZI** | | | | | |
| Kumtafuta Mshauri Elekezi wa kukamilisha ripoti ya uzalishaji umeme wa jua na kihifadhio cha nishati ya umeme (*Consultancy services for design, procurement support and supervision of the solar PV generation plant and battery energy system (BESS) LUMPSUM)* | ripoti ya uzalishaji umeme iliotayarishwa | 100 | 100% | 100% | Ripoti (Feasibility Study) ya solar pv na BESS zimekamilika. Aidha, tathmini ya kiufundi (technical evaluation) kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayesambaza na kufunga mitambo ya kuhifadhia umeme (BESS) imekamilika. |
| usimamizi wa ujenzi wa kituo cha uzalishaji umeme wa jua na kihifadhio cha nishati ya umeme (*supervision of installation of the solar PV generation plant and battery energy system (BESS) TIME – BASED)* | Asilimia ya Ujenzi wa Kituo. | 100 | 15% | 15% | Ujenzi wa ukuta kwa ajili ya solar PV umekamilika. *taratibu* za manunuzi kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi wa mtambo wa wa umeme wa jua na kihifadhio cha umeme (BESS). |
| Mshauri Elekezi kukamilisha ripoti ya SCADA *(Consultancy services for supervision and monitoring of the SCADA (LUMPSUM))* | Asilimia ya Ripoti ya SCADA iliyokamilishwa | 100 | 100% | 100% | Ripoti imekamilika. |
| Mshauri Elekezi kusimamia ujenzi wa SCADA *(Consultancy services for supervision and monitoring of* | Asilimia ya Ujenzi wa SCADA | 100 | 15% | 15% | Hatua za manunuzi za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kufunga mitambo ya kidigitali ya |

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| *the SCADA (TIME - BASED))* | | | | | kusimamia miundombinu ya umeme zimekamilika. Shirika la umeme (ZECO) tayari limeshasaini mkataba na kampuni ya NARI-NR ya China tarehe 15 Julai, 2025 na Kampuni hiyo imeanza kazi ya kukusanya taarifa kwa ajili ya usanifu (design). |
| Mshauri Elekezi kukamilisha ripoti ya miundombinu ya umeme wa mkondo wa kilovoti 132 na vituo vya kupoozea umeme (*Consultancy services for supervision and monitoring of the 132kv backbone transmission and substation infrastructure works (Time-based).* | Asilimia ya Ripoti ya Miundombinu. | 100 | 40% | 40% | Mkandarasi wa njia ya umeme amekamilisha upimaji wa njia ya umeme yenye urefu wa kilometa 100, pamoja na geotechnical survey kwenye maeneo yote ya nguzo za kwenye kona. |
| Mshauri Elekezi kusimamia ujenzi wa uwekaji na uboreshaji wa miundombinu ya ndani ya umeme (Consultancy services for distribution network investments and access scale-up activities (TIME-BASED). | Asilimia ya Ujenzi na Uwekaji na Uboreshaji wa Miundombinu. | 100 | 0 | 0 | Hatua za manunuzi kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa uwekaji na uboreshaji wa miundombinu ya ndani ya umeme zinaendelea. |

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Automatic Meter Reading (AMR) Integration of billing software. | Asilimia ya Kukamilisha mifumo ya utoaji bili | 100 | 100 | 100 | Mafunzo kwa wataalamu wa ZECO kwa ajili ya ujengaji uwezo maswala ya bili yalishafanyika kwa mujibu wa Mkataba. Aidha, ZECO itaingia mkataba mfupi na Kampuni ya HEXING ya China ambayo itasaidia katika kukamilisha mfumo wa taarifa za wateja. |
| **USANIFU, UNUNUZI NA UJENZI (ENGINEERING, PROCUREMENT AND CONSTRUCTION WORKS** | | | | | |
| Usanifu, ununuzi na uwekaji wa miundombinu ya uhifadhi wa nishati ya umeme *(Design, supply and installation of the proposed battery energy storage system (BESS).* | Asilimia ya uwekaji miundombinu iliofikiawa | 100 | 15 | 15 | Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi na kukamilisha usanifu (design). Aidha, usafishaji wa maeneo umekamilika. Kwa upande wa vituo vya kupozea umeme (substation), mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi (civil works) katika vituo vya Welezo, Makunduchi na Matemwe. |
| Usanifu, ununuzi na ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji | Asilimia ya Ujenzi wa | 100 | 15 | 15 | Eneo la ujenzi wa kituo cha solar pv linaendelea |

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| umeme kwa kutumia nishati ya jua *(Design, supply and installation of the proposed solar PV generation plant).* | Miundombinu | | | | na kazi ya ujenzi wa ukuta, upimaji wa geotechnical survey, topographic survey, kusafisha eneo na ujenzi wa barabara (access road) |
| Usanifu,ununuzi na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 132 *(Design, supply, and installation of the proposed 132kV backbone transmission line infrastructure)* | Asilimia ya kazi ya Usanifu iliofanyika | 100 | 25 | 25 | Mkandarasi anaendelea na usanifu wa njia ya umeme (designs), ufyekaji wa njia ya umeme, amekamilisha upimaji na kukamilisha geotechnical investigation kwenye nguzo za kona. Anaedelea na *geotechnical investigation* kwenye baadhi ya *suspension towers locations*. |
| Matemwe (132/33kV) na Makunduchi (132/33kV (Design, supply, and installation of the proposed 132kV backbone transmission substations at Welezo, Matemwe, and Makunduchi). Matemwe (132/33kV) na Makunduchi | Asilimia ya Ujenzi wa Vituo iliyofanyika | 100 | 40 | 40 | Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa vituo vya usambazaji umeme kwa ajili ya kuweka mitambo. |

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| (132/33kV (Design, supply, and installation of the proposed 132kV backbone transmission substations at Welezo, Matemwe, and Makunduchi). | | | | | |
| Usanifu, ununuzi na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kati na mdogo kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya ndani. *(Design, supply and installation of the proposed medium voltage and low voltage network extension and strengthening works)* | Asilimia ya Ujenzi ilofanyika | 100 | 15 | 15 | Mradi unaendelea na tathmini (evaluation) kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kuweka miundombinu ya kusambazia umeme. Ripoti ya tathmini imewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupatiwa Ridhaa (No-Objection). |
| Usanifu, ununuzi na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa ukusanyaji wa taarifa za matumizi ya umeme *(SCADA/EMS (Design, supply and installation of the proposed SCADA/EMS system)* | Asilimia ya Ujenzi | Kuanza kwa ujenzi wa kituo cha SCADA katika eneo la Mtoni | 15 | 15 | Mkandarasi anaendela kukusanya taarifa kwa ajili ya usanifu wa mfumo wa SCADA zitakazosaidia utayarishaji wa zabuni ya ujenzi wa SCADA. |
| Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi. | Idadi ya watu waliolipwa fidia | 1510 | 1354 | 96 | Wizara tayari imelipa fidia kwa waathirika wa mradi na inaendelea kupokea taarifa za benki kwa waathirika waliobakia ambao taarifa |

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | zao hazijakamilika ili kufanya malipo. |
| Utoaji wa mafunzo ya shughuli za uhamishaji wa wananchi katika maeneo ya mradi. | Asilimia ya mafunzo yaliyotolewa | 100 | 100 | 100 | Mafunzo yametolewa kwa wananchi katika maeneo ya mradi; |
| Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkuu wa Umeme wa Miaka ishirini. | Asilimia ya Ripoti ya Mpango Mkuu | 100 | 95 | 95 | Ripoti ya Mpango Mkuu wa Umeme imekamilika. |
| Kuanda Mpango wa Bei ya Umeme kwa ZURA | Asilimia ya Mpango wa Bei | 100 | 100 | 100 | Ripoti imekamiika |

**Kiambatisho Namba 10: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| KAZI ZA KAWAIDA | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MSHAHARA (PE)** | **RUZUKU YA MSHAHARA** | **UENDESHAJI WA OFISI (OC)** | **MAKISIO YA SMZ** | **MHISANI** | **RUZUKU** | **MAPENDEKEZO YA 2026/2027** |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI** | **362,740,000** | **9,218,310,000** | **2,101,600,000** | **116,358,954,254** | **38,893,761,625** | **12,984,823,533** | **179,920,189,412** |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji | 362,740,000 | 9,218,310,000 | 2,101,600,000 | 116,358,954,254 | 38,893,761,625 | 12,984,823,533 | 179,920,189,412 |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI** | **458,000,000** | **-** | **332,638,580** | **199,062,445,746** | **82,515,121,592** | **9,003,720,250** | **291,371,926,168** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | 458,000,000 | | 287,217,580 | 197,562,445,746 | 82,515,121,592 | 9,003,720,250 | 289,826,505,168 |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini | | | 45,421,000 | 1,500,000,000 | | | 1,545,421,000 |
| **URATIBU WA MIPANGO, UENDESHAJI NA UTAWALA WA WMNM** | **2,150,260,000** | **-** | **1,951,351,420** | **-** | **-** | **-** | **4,101,611,420** |
| Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za WMNM | 230,000,000 | | 630,380,000 | | | | 860,380,000 |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | 1,419,470,000 | | 764,781,420 | | | | 2,184,251,420 |
| Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM - PEMBA | 500,790,000 | | 556,190,000 | | | | 1,056,980,000 |
| **JUMLA KUU** | **2,971,000,000** | **9,218,310,000** | **4,385,590,000** | **315,421,400,000** | **121,408,883,217** | **21,988,543,783** | **475,393,727,000** |


Zanzibar Government Printing Press Agency